

**VIAMBISHI NJEO KATIKA VITENZI VYA LAHAJA YA KIPEMBA:
UCHANGANUZI WA KIMOFOFONOLOJIA KUONESHA MUUNDO
NDANI NA MUUNDO NJE**

HALIMA SALIM ABDULLA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHAHADA
YA UMAHIRI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU
HURIA CHA TANZANIA**

2016

UTHIBITISHO

Aliyetia saina hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii iitwayo *Viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba: Uchanganuzi wa kimofonolojia kuonesha muundo ndani na muundo nje* na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa shahada ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....
DKT: P. P. LIPEMBE

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile kieletroniki, kurudufu nakala , kurikodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria kwa niaba.

TAMKO

Mimi Halima Salim Abdulla nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote.

.....
Halima Salim Abdulla

.....
Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa watoto wangu wapenzi na baba yangu mpenzi bwana Salim Abdulla kwa kunilea na kunisomesha hadi kufikia kiwango hiki cha elimu.

SHUKRANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa mbingu na ardhi kwa kunijaalia uhai, uzima , kunipa uwezo wa kufanya utafiti, kuandika na kuikamilisha kazi hii. Pili napenda niwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine kukamilika kwa kazi hii. Hata hivyo si rahisi kuwataja wote kwa majina ila ninapenda kuwashukuru wote nitakaowataja na ambao sijawataja kwa mchango wao wa kuifanikisha kazi hii. Shukrani za pekee ziende kwa msimamizi wangu Dkt. P.P.Lipembe kwanza kwa kunishawishi kuendelea na masomo, pili kwa kukubali kuwa msimamizi wangu, tatu kwa moyo wake wa kunihimiza kufanya kazi kila alipohisi kuwepo kwa ugumu na namna fulani ya kusita na kuchelewesha kazi. Aidha ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kuanzisha kozi hii hapa kituoni petu Pemba. Shukrani zangu maalum ziwaendee wazazi wangu wapendwa; baba yangu na mama yangu kwa mapenzi yao na huruma kubwa zilizowapelekea kunilea kwa uangalifu mkubwa na kunisomesha hadi kufikia elimu ya juu. Nitakuwa mwizi wa shukrani na mchawi wa fadhila iwapo nitawacha kumshukuru mume wangu mpenzi pamoja na watoto wangu wapendwa kutokana na ustahamilivu walioonyesha muda wote niliokuwa nikiwakosesha haki walizostahili kutokana na harakati za kufanya utafiti na uandishi wa kazi hii ngumu na yenye kuhangaisha fikra na akili. Nawashukuru niliowataja na kwa niaba ya nisiowataja nyote ninawambieni ahsanteni sana.

IKISIRI

Kazi hii inachambua mofofonolojia ya vitenzi vya lahaja ya Kipemba kuonesha muundo ndani na muundo nje . Utafiti ulilenga ubainisha mambo matatu; kwanza kuchunguza viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba; pili kueleza michakato ya kimofofonolojia inayojitokeza katika kubadilisha miundo ndani na miundo nje; na tatu kudhihirisha kanuni zinazotawala mabadiliko ya muundo ndani na muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Utafiti huu ulifanyika katika Shehia ya Mtambwe Kaskazini katika jimbo la Mtambwe ambalo lilihusisha kijiji cha Kele, Uondwe, Mpakanjia, Jambaji, Kiapaka na Chanjaani. Watoa taarifa za utafiti walikuwa wakaazi asilia wa Mtambwe Kaskazini wenye umri kati ya miaka sitini nakuendelea ambao waliteuliwa kumi kutoka kila kijiji kwa njia ya usampulishaji bahati nasibu. Mbinu mbalimbali za utafiti zilitumika katika utafiti huu zikiwemo mbinu ya dodoso, usaili na uchunguzi makini. Matokeo ya utafiti yameonyesha michakato ya kimofofonolojia inavyojitokeza kwenye mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba na kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko yanayotokea kutoka muundo ndani kwenda muundo nje katika vitenzi vya lahaja za Kipemba.

YALIYOMO

<u>UTHIBITISHO</u>	i
<u>HAKI MILIKI</u>	ii
<u>TAMKO</u>	iii
<u>TABARUKU</u>	iv
<u>SHUKRANI</u>	v
<u>IKISIRI...</u>	vi
<u>YALIYOMO</u>	vii
<u>ORODHA YA MAJEDWALI</u>	xi
<u>SURA YA KWANZA</u>	1
<u>UTANGULIZI NA USULI WA UTAFITI</u>	1
<u>1.1 Utangulizi</u>	1
<u>1.2 Lahaja ya Kipemba</u>	2
<u>1.3 Dhana ya Mofofonolojia</u>	5
<u>1.4 Kanuni za Kimofonolojia</u>	5
<u>1.4.1 Uyeyushaji (Glide formation)</u>	6
<u>1.4.2 Udondoshaji wa Irabu (Vowel deletion)</u>	7
<u>1.4.3 Tangamano la Irabu (Vowel harmony)</u>	7

<u>1.5 Vitenzi</u>	7
<u>1.6 Viambishi</u>	8
<u>1.7 Dhana ya Njeo</u>	8
<u>1.7.1 Kiambishi Njeo</u>	9
<u>1.7.2 Viambishi Njeo vya Kiswahili</u>	9
<u>1.9 Usuli wa Mada</u>	15
<u>1.10 Tatizo la Utafiti</u>	16
<u>1.11 Malengo ya Utafiti</u>	17
<u>1.11.1 Lengo Kuu</u>	17
<u>1.11.2 Malengo Mahsusi</u>	17
<u>1.11.3 Maswali ya Utafiti</u>	18
<u>1.12 Umuhimu wa Utafiti</u>	18
<u>1.13 Mawanda ya Utafiti</u>	19
<u>1.14 Changamoto za Utafiti huu na Suluhu Zake</u>	19
<u>SURA YA PILI</u>	21
<u>MAPITIO YA KAZI TANGULIZI</u>	21
<u>2.1 Utangulizi</u>	21
<u>2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Muundo wa Vitenzi Vinavyozungumzia Viambishi Njeo</u>	
22	
<u>2.3 Kiunzi cha Nadharia</u>	25
<u>2.4 Muhtsari wa Sura</u>	26
<u>SURA YA TATU</u>	28

<u>MBINU ZA UTAFITI</u>	28
<u>3.1 Utangulizi.</u>	28
<u>3.2 Muundo wa Utafiti</u>	28
<u>3.3 Eneo la Utafiti</u>	29
<u>3.4 Watoa Taarifa</u>	29
<u>3.4.1 Sampuli na Usampulishaji</u>	30
<u>3.5 Mbinu za Kukusanyia Data</u>	31
<u>3.5.1 Dodoso</u>	31
<u>3.5.2 Uchunguzi Makini</u>	33
<u>3.5.3 Mbinu ya Usaili</u>	34
<u>3.6 Mbinu za Kuchambua na Kufafanua Data</u>	35
<u>3.7 Misingi ya Maadili ya Utafiti</u>	36
<u>3.8 Muhtasari wa Sura</u>	37
<u>SURA YA NNE</u>	38
<u>UWASILISHAJI, UFAFANUZI NA UCHANGANUZI WA DATA</u>	38
<u>4.1 Utangulizi</u>	38
<u>4.2 Viambishi Njeo Katika Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba</u>	38
<u>4.2.1 Kiambishi Njeo cha Wakati Uliopo katika Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba</u>	40
<u>4.2.2 Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Hali Timilifu</u>	43
<u>4.2.3 Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Wakati Uliopita</u>	44
<u>4.2.4 Kiambishi Njeo cha Wakati Ujao</u>	45
<u>4.2.5 Kiambishi Kinachowakilisha Hali ya Kudadisi kwa Tendo</u>	46

<u>4.2.6 Kiambishi cha Hali ya Mazoea</u>	48
<u>4.3 Michakato Ya Kimofonolojia Kwenye Viambishi Njeo</u>	49
<u>4.3.1 Michakato ya kimofonolojia kwenye njeo ya wakati timilifu</u>	56
<u>4.3.2 Michakato ya Kimofonolojia kwenye Njeo ya Wakati Uliopo</u>	57
<u>4.3.3 Michakato ya Kimofonolojia kwenye Hali ya Kudadisi kwa Tendo</u>	59
<u>4.3.4 Michakato ya Kimofonolojia kwenye Vitenzi vya Hali ya Mazoea.</u>	60
<u>4.4 Kanuni Zitumikazo Kugeuza Miundo Ndani kwenda Miundo Nje</u>	60
<u>4.4.1 Kanuni Zitumikazo kwenye Njeo ya Wakati Uliopita</u>	60
<u>4.4.1.1 Udondoshaji</u>	60
<u>4.4.1.2 Uyeyushaji</u>	61
<u>4.4.2 Kanuni Zinazotumika kwenye Njeo ya Wakati Timilifu na Wakati Ujao</u>	63
<u>4.4.3 Kanuni Zinatumika kwenye Njeo ya Wakati Uliopo</u>	63
<u>4.4.4 Kanuni za Mabadiliko ya Kimofonolojia katika Muundo wa Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba (kudadisi kwa tendo)</u>	65
<u>4.4.5 Kanuni Zitumikazo kwenye Hali ya Mazoea</u>	66
<u>4.4.6 Muhtasari wa Sura</u>	66
<u>SURA YA TANO</u>	68
<u>MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO</u>	68
<u>5.1 Muhutasari wa Utafiti</u>	68
<u>5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti</u>	69
<u>5.3 Hitimisho</u>	70
<u>5.4 Mapendekezo ya Utafiti</u>	70

<u>5.4.1</u> <u>Mapendekezo ya Utekelezaji</u>	71
<u>5.4.2</u> <u>Mapendekezo ya Tafiti Nyingine</u>	71
<u>MAREJELEO</u>	72
<u>VIAMBATANISHO</u>	75

ORODHA YA MAJEDWALI

<u>Jedwali Na. 1.1: Viambishi Njeo vya Kiswahili</u>	10
<u>Jedwali 1.2: Viambishi njeo vya Kiswahili</u>	14
<u>Jedwali 1.3: Konsonanti na Viyeyusho katika Lahaja ya Kipemba</u>	14
<u>Jedwali 2.1: Tofauti za Viambishi Njeo baina ya Kipemba na Kiswahili Sanifu</u>	23
<u>Jedwali 2.2: Njeo za Nyakati Mbali Mbali katika Kiswahili</u>	24
<u>Jedwali 4.1: Mifano ya Viambishi Njeo katika Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba</u>	39
<u>Jedwali 4.2. Kiambishi kinachowakilisha Njeo ya Wakati Uliopo (Uyakinishi)</u>	41
<u>Jedwali 4.3: Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Wakati Uliopo (Ukanushi)</u>	42
<u>Jedwali 4.4: Kiambishi cha Wakati Timilifu Kuwakilisha Njeo Uyakinishi na Ukanushi</u>	43
<u>Jedwali 4.5: Njeo za Wakati Uliopita katika Hali ya Uyakinishi</u>	44
<u>Jedwali 4.6: Kiambishi Njeo cha Wakati Uliopita (Hali ya Ukanushi)</u>	45
<u>Jedwali 4.7: Kiambishi kinachowakilisha Njeo ya Wakati Ujao Ukanushi</u>	46
<u>Jedwali 4.8: Kiambishi Kinachowakilisha Hali ya Kudadisi kwa Tendo katika Kipemba</u>	47
<u>Jedwali 4.9: Kiambishi cha Hali ya Mazoea</u>	48
<u>Jedwali 4.10: Vitenzi Vinavyoonyesha Njeo ya Wakati Yakinishi Uliopita kwa Nafsi ya Kwanza Umoja</u>	50
<u>Jedwali 4.11: Tofauti ya Sentensi za Kipemba zenye Kiambishi cha Njeo ya Wakati Uliopita (yakinishi)</u>	51

<u>Jedwali 4.12: Tofauti za Miundo ya Nje, kwenye Sentensi za Kipemba</u>	
<u>Zinazoonyesha Wakati Uliopita kwa Nafsi ya Kwanza Uwingi, Nafsi ya</u>	
<u>Pili Uwingi na Nafsi ya Pili Umoja</u>	52
<u>Jedwali 4.13: Vitenzi vya Kawaida Vilivyoambikwa Njeo ya Wakati Uliopita</u>	
<u>(ukanushi) kwenye Nafsi ya Kwanza hadi ya Tatu Umoja na Uwingi</u>	54
<u>Jedwali 4.14: Michakato ya Kimofonolojia kwenye Njeo ya Wakati Timilifu</u>	57
<u>Jedwali 4.15: Vitenzi vya Silabi Moja Vilivyoambikwa Njeo ya Wakati Uliopo</u>	58
<u>Jedwali 4.16: Michakato ya Kimofonolojia kwenye Hali ya Kudadisi kwa tendo</u>	59
<u>Jedwali 4.17: Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Wakati Timilifu na Wakati Ujao</u>	

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA USULI WA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo inatoa taarifa za awali zinazohusu mada ya utafiti na imegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusiana na usuli wa mada. Aidha sehemu ya pili inabainisha tatizo la utafiti. Sehemu ya tatu inaweka bayana malengo ya utafiti na maswali yaliyomuongoza mtafiti kuweza kuyafikia malengo aliyokusudia. Halikadhalika sehemu ya nne inazungumzia umuhimu wa utafiti. Sehemu ya tano inabainisha mawanda ya kitaaluma na mipaka yake na sehemu ya sita inazungumzia juu ya changamoto mbalimbali za utafiti na suluhu zake.

Katika sura hii utafiti huu umechunguza viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya kipemba kwa lengo la kuchunguza michakato ya kimofonolojia kuonesha muundo ndani na muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba kwa kupitia kanuni zinazotawala mabadiliko ya kimofonolojia kuonesha muundo ndani na muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba.

Pia sura hii inachambua na kujadili dhana mbali mbali zinazohusu mada ya viambishi njeo kwa ujumla na viambishi njeo katika lugha mahsusi. Mada zinazojadiliwa ni pamoja na; dhana ya lahaja za Kipemba, dhana ya kitenzi, dhana ya

njeo, dhana ya viambishi, dhana ya viambishi njeo, dhana ya mofofonolojia, kanuni za kimofonolojia vile vile na dhana ya umbo ndani na umbo nje.

1.2 Lahaja ya Kipemba

Lahaja ya Kipemba ni lahaja ya Kiswahili inayoongelewa katika eneo lote la Kisiwa cha Pemba isipokuwa eneo la kusini la kisiwa hicho ambako inasemekana kunaongelewa lahaja ya Kitumbatu. Kipemba hakijafanyiwa utafiti kwa kiwango kikubwa sana, hata hivyo zipo kazi chache zilizofanywa na kudiriki kuibua hisia na mitazamo mbalimbali. Miongoni mwa mitazamo hiyo ni ule mtazamo au fikra isemayo kwamba Kipemba hakina mgawanyiko kwa hivyo Pemba yote inatumia lahaja moja tu isiyo na mabadiliko ndani yake. Wataalamu wanaoliamini na kulikubali wazo hilo ni Stigand (1915) na Mkude (1983). Baadhi ya wataalamu kama Whiteley (1958) anafikiria kwamba katika kisiwa cha Pemba kuna lahaja zaidi ya moja ambazo zinaongelewa kisiwani humo. Whitely (keshatajwa) anafikiri kwamba maeneo ya kaskazini mashariki ya Pemba (Micheweni – Wingwi) Katika kisiwa cha Kojani na eneo la Matele – Kiuyu; kusini mwa Kojani kuna tofauti za uzungumzaji ambazo zinabeba hadhi ya kuitwa kuwa ni lahaja tofauti. Ushahidi ameukita kwenye madai yanayoonyesha tofauti ya baadhi ya vipashio vya kisarufi. Kwa mfano, kiwakilishi cha kuonyesha kitu kilicho karibu ‘hiki/hapa’. Alitoa mifano ya vijiji vya Matele, Kambini, Chokocho na Micheweni. Pamoja na ukweli huo, eneo hilo mtafiti hatojishughulisha nalo na wala hatolifanyia utafiti kwa kuwa sio analokusudia kulifanyia utafiti.

Whiteley (keshatajwa) aliwahi kuandika kazi inayohusiana na lahaja ya Kipemba na akajihusisha na uchambuzi wa vipengele vingi zikiwemo ngeli mbalimbali za nomino za lahaja hiyo, tarakimu kumi za mwanzo, viwakilishi, viwakilishi vimilikishi, viaangama kwenye lahaja ya Kipemba, viwakilishi vya kuonyesha, alama ya mtendwa, njeo na hali mbalimbali. Pia amebainisha msamiati wa Kipemba, katika kiwango cha neno na maana yake. Kazi hii ilihusu lahaja ya Kipemba, haikuhusika na ulinganishaji na utofautishaji kati ya lahaja hii ya Kipemba na lahaja nyingine. Mtafiti anahisi kwamba kazi ya Whiteley (keshatajwa) ni ya maana na itakuwa kielelezo na mwongozo katika kubaini vipengele vya msingi kama mfumo wa sauti, muunganiko wa sauti na tofauti za utokeaji wa uyeyushaji wa kiisimu, tofauti za ngeli za nomino, tofauti ya matumizi ya tarakimu, viwakilishi vya aina mbalimbali na viangama, tofauti ya alama ya njeo za wakati na athari zake na tofauti kati ya alama za mtenda na mtendwa, tofauti za kimsamiati na kimaana, vitu vinavyohitajika hapa ni kutofautishwa baina ya lahaja mbili ambazo ni lahaja ya Kipemba na lahaja ya Kitumbatu.

Sacleux (1909:1) anaeleza Kipemba kina lahaja ndogo nne (4) na kazitaja kama ifuatavyo:

Kipemba cha Kusini, Kipemba cha Kivitongoji Mvumoni, Ki-Chake Chake cha Chake Chake na Kimsuka cha Chaleni. (*Tafsiri ni ya mtafiti*) Katika kazi yake hiyo anaeleza matumizi ya kiambishi “ki-” kinachotumika katika Kipemba badala ya “ch-”. Mfano “*kyombo kyema*” badala ya “*chombo chema*”. Hata hivyo, kazi yake ina walakini kwani haibainishi kwa kina tofauti za kiisimu za lahaja hizo. Kwa

upande wa mgao wa lahaja, pia lahaja zote alizotaja ziko kusini isipokuwa Kimsuka cha Chaleni.

Naye Stigand (1915) katika kazi yake anatoa maelezo machache kuhusu “Lahaja ya Kipemba”. Zaidi anaangalia msamiati wa Kipemba unavyofanana au kutofautiana na lahaja nyingine za Kiswahili. Dondoo lifuatalo linafafanua:

Kipemba ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Inafanana na lahaja ya zamani, kina maneno mengi yaliyochukuliwa kutoka wakazi wa zamani wa visiwani” (*Tafsiri ni ya mtafiti*).

Hata hivyo, kazi ya Stigand haina uchambuzi wa kiisimu wa Kiswahili kizungumzwacho katika maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Kipemba.

Polome (1967) alitafiti na kuandika juu ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake. Katika kazi yake anabainisha kuwa Micheweni wanazungumza lahaja ndogo ambayo kwa kiasi fulani inatofautina na maeneo mengine ya Pemba. Polome (1967:24) anafafanua: Kipemba kinazungumzwa katika Kisiwa cha Pemba isipokuwa Pemba Kusini ambako hakuna ukaakaishaji wa kiambishi ki- kabla ya nomino zinazoanza na irabu. Katika baadhi ya maeneo kama Micheweni-Wingwi pembe ya Kaskazini, lahaja ndogo zimetokea; kwa mfano, Micheweni wanatumia ‘k-’ badala ya ‘h-’ katika kiambishi cha ukanushi wa nafsi ya pili au ya tatu umoja. (*Tafsiri ni ya mtafiti*).

Polome amejaribu kuonyesha tofauti ya uzungumzaji baina kusini na kaskazini ya Kisiwa cha Pemba ingawa hakutoa mifano wala hakufanya uchanganuzi wa vipengele vya kiisimu vya lahaja alizozungumzia ili kubainisha tofauti hizo. Kazi iliyofanywa kuhusiana na uchambuzi wa lahaja za Kiswahili kwa undani kidogo ni ile ya Maganga (keshatajwa) iliyolinganisha na kutofautisha kati ya lahaja za visiwani, yaani Kiswahili sanifu, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba. Kazi hii ilijihusisha zaidi na vipengele vya kimofonolojia ikiachia mbali vipengele vingine hasa vya kimsamiati kuwepo mlingano wa maumbo na tofauti za kimaana, kuwepo mlingano wa maana katika maumbo tofauti kuwepo maumbo yanayolingana hali ya kutofautiana baadhi ya sauti, ambavyo mtafiti kwa maoni yake anahisi ni eneo muhimu na la kuvutia kufanyia uchunguzi.

1.3 Dhana ya Mofonolojia

Kwa mujibu wa Massamba (1996) mofonolojia ni tawi la isimu linayohusu mchakato wa kimuingiliano kati ya mofolojia na fonolojia. Mchakato huu unajishughulisha na athari zinazojitokeza kwenye mpaka wa mofu mbili pale mofu hizo zinapokutana. Uchunguzi wa kimofonolojia unachunguza mchakato na kanuni ambazo hutabiri mabadiliko ya sauti zinazounda mofimu katika lugha fulani. Kanuni hizo zinaweza kubadilisha muundo ndani kwenda muundo nje ambao ndio unaosikika kutoka kwa muongaji wa lugha fulani. Vipengele vinavyounda mofimu katika muundo ndani ambao unaitwa mofonimu. Muundo nje unaotokana na

kanuni za kimofonolojia zenye kanuni (ambazo baadaye hufuata kanuni za kifonolojia zilizozeleka ili kutoa sauti mpya za kifonetiki).

1.4 Kanuni za Kimofonolojia

Kwa mujibu wa Goldsmith (1995) kanuni za kimofonolojia ni mpango mahsusi unaotumika kuwasilisha michakato ya kifonolojia au kimofonolojia katika lugha. Kanuni hizi ni mashuhuri na zaidi hutumika kwenye taaluma ya fonolojia zalishi kuonyesha uhusiano wa sauti iliyodhihiri kwenye muundo nje jinsi inavyoakisiana na tafsiri ya ubongo wa muongaji pale alipoifasili kutoka muundo ndani. Akifafanua zaidi Goldsmith (1995) amezelezea kanuni za kimofonolojia kuwa ni dira maalum inayozihusisha katika ngazi tofauti za utamkaji wa sauti. Yaani, ni dira inayoongoza mchakato wa mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje.

Kwa upande mwingine, Bruce Hayes (2009) ameelezea kuwa kanuni za kimofonolojia ni mkusanyiko wa njia mbalimbali zinazoshughulikia sauti na jinsi zinavyoathiriana kutegemeana na mazingira zinamozalishwa. Hii inamaana kwamba kanuni za kifonolojia zinaelezea jinsi mzungumzaji anawasilisha kile kilichofichikana ubongoni kwa kutumia sauti chache alizoamua kuzidhihirisha kutokana na sauti nyingi zilizounda muundo ndani. Kanuni za kimofonolojia kikawaida huanza kuzibadilisha kwa kuzichunguza sauti zilizounda muundo nje na kuzitizama jinsi zilivyoathiriana ili hatimaye kupatikane muundo ndani.

Hooper (1972) amesema kwamba kanuni za kimofofonolojia hujitokeza kwenye mipaka ya mofu mbili wakati sauti mbili zinapokutana kuathiriana kifonetiki na kuambukizana sifa zao. Miongoni mwa kanuni za kimofofolojia zinazotarajiwa kujitokeza katika mazingira tofauti tofauti, kutawala miundo ndani ili kusababisha kutokea kwa miundo nje ni:

1.4.1 Uyeyushaji (Glide formation)

Dhana ya kanuni ya uyeyushaji imeelezwa na Massamba na wenzake (2003:25) kuwa ni hali inayojitokeza endapo irabu **u** au **i** inafanana kabisa na irabu hizo basi irabu **u** na irabu **i** hubaki kama ilivyo, endapo irabu inayozifuatia irabu hizo haifanani na hizo basi irabu hizo hubakia kama zilivyo au huyeyuka na kuwa kiyeyusho. Mfano neno m [u...e...] nde...sha...ji huwa mwendeshaji.

1.4.2 Udondoshaji wa Irabu (Vowel deletion)

Dhana ya udondoshaji wa irabu imeelezwa na Mgullu(1999:90) kuwa ni hali ambapo irabu mbili au zaidi zinazofanana huwa zimefuatana, penye shadda la irabu kuliko mahali pengine popote ambako hakuna shadda lolote la irabu, irabu hudondoshwa hasa kwenye nomino,vivumishi,vitenzi na viwakilishi.Mfano kwenye nomino wa+anafunzi - wanafunzi. Kilichotokea hapa ni kuwa irabu **a** imedondoshwa kwenye nomino waanafunzi na kubaki wanafunzi.

1.4.3 Tangamano la Irabu (Vowel harmony)

Mgullu (1999:92) anaeleza tangamano la irabu kuwa ni utaratibu wa irabu fulani kukubali kuandamana katika mazingira maalum. Katika Kiswahili tangamano la irabu hujitokeza katika baadhi ya viambishi tamati vya vitenzi. Kwa mfano, katika mofu za mofimu za kutendesha tunaona kwamba zinabadilikabadilika ambako kunasababishwa na irabu iliyo katika mzizi wa kitenzi, irabu zinazotumika katika mnyambuliko ni mbili ambazo ni / i / na / e /. Kwa mfano, endapo mzizi wa kitenzi una irabu / a / , / i / na / u / mnyambuliko unatakiwa uwe na irabu / i /. Mfano (andik) – (andik) + (ish) + (a) – andikisha. Endapo mzizi wa kitenzi una irabu / o / na / e / basi mnyambuliko unatakiwa uwe na irabu / e /. Mfano (chez) – (chez) + (esh) + (a) – chezsha.

1.5 Vitenzi

Kwa mujibu wa Mgullu (1999) vitenzi ni aina ya maneno ambayo hutumika katika sehemu muhimu sana ya kiarifu cha sentensi na ambayo huarifu / hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi.

Kihore na wenzake (2003) wanasema kuwa kitenzi ni aina ya neno inayotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Fasili hii ya Kihore inaungwa mkono nakusisitizwa na Habwe na Karanja (2004). Katika lugha ya Kiswahili vitenzi ni maneno pekee ambayo ni lazima yawepo katika sentensi ndipo sentensi iweze kuwa sentensi.

1.6 Viambishi

Kihore na wenzake (2003) wanasema kuwa kiambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Pia wanaeleza kuwa viambishi katika lugha ya Kiswahili huweza kujitokeza tu mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa vitenzi. Wanaeleza kuwa Kiswahili hakina viambishi kati. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa vitenzi huitwa viambishi awali, ilhali vile ambavyo huwekwa katikati ya mzizi huitwa viambishi kati na vile ambavyo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa viambishi vifuatilizizi. Ukweli ni kuwa Kiswahili hutumia viambishi vya aina mbili tu yaani viambishi awali na viambishi tamati.

1.7 Dhana ya Njeo

Njeo ni kategoria ya kisarufi ambayo huwakilisha muda au wakati tendo hufanyika. Njeo hueleza uhusiano ulioko baina ya wakati wa kutamka na wa kutenda. Njeo katika Kiswahili huelezwa na kitenzi Habwe na Karanja (2004) wakiinukuu Tuki (1990). Njeo katika lugha ya Kiswahili hutumika kwa maana ya wakati ambapo tendo lilitendeka au halikutendeka. Kiswahili kina njeo iliyopita, njeo iliyopo na njeo ijayo.

1.7.1 Kiambishi Njeo

Kiambishi njeo ni kiambishi kinachowakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahsusuni. Kila lugha ina mfumo wake wa kuwasilisha kiambishi cha aina hiyo. Katika lugha ya Kiswahili kiambishi hicho huwasilishwa na mofu maalumu inayojitokeza baada ya kiambishi nafsi. Wataalamu mbali mbali kama Habwe na Karanja (2004),

Massamba na wenzake (2003), Mgullu (1999) amelezea dhana ya kiambishi njeo, kwa majina tofauti tofauti.

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (weshatajwa) kiambishi njeo ni mofu inayowakilisha mofimu ya wakati. Kwa upande mwingine Massamba na wenzake (washatajwa), wamekiita kiambishi hiki kuwa ni mofimu ya njeo. Naye Mgullu (keshatajwa) amekiita kiambishi hiki kwa jina hilo hilo. Wote kwa ujumla wamewafikiana kuwa: kiambishi njeo ni kiambishi awali kinachowakilisha wakati katika kitenzi. Katika kazi hii kiambishi njeo kinatafsiriwa kuwa ni kijumbo kidogo au mofu iliyondani ya kitenzi inayowakilisha mofimu ya wakati.(Tafsiri ya mtafiti)

1.7.2 Viambishi Njeo vya Kiswahili

Kitenzi cha Kiswahili pia huchukua mofimu ya njeo. Mofimu ya njeo pia ni kiambishi awali, kumaanisha kuwa mofimu hii huja kabla ya mzizi wa kitenzi (Habwe na Karanja weshatajwa). Viambishi njeo katika lugha ya Kiswahili huambikwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. Kihore na wenzake (2003) wameorodhesha viambishi njeo katika Kiswahili kama inavyoonyeshwa hapo chini (Kihore na wenzake 2003).

Jedwali Na. 1.1: Viambishi Njeo vya Kiswahili

Njeo	Mfano wa kiambishi	kitenzi	mtindo wa kitenzi
Wakati uliopo	-na-	- unase	kukubali

Wakati uliopo	-i-	hatulii	kukanusha
Wakati uliopita	-li-	alikuja	kukubali
Wakati uliopita	-ku-	hakulia	kukanusha
Wakati ujao	-ta-	atakuja	kukubali
Wakati uliopita hali timilifu	-me-	amerudi	kukubali
Hali ya mazoea	-hu-	humsaidia	kukubali

1.8 Dhana ya Umbo Ndani na Umbo Nje la Maneno

Dhana za msingi katika utafiti huu za muundo ndani na muundo nje. Dhana hizi zinazotumika katika isimu hasa kwenye somo la sintaksia kama ilivyoelezwa na Chomsky (1957). Muundo ndani katika isimu ni nadharia ya kimuundo inayohusisha miundo ya sentensi katika sintaksia na miundo ya maneno katika mofolojia. Dhana hii ilielezwa na kutiliwa mkazo sana na mwanaisimu aliyeitwa Chomsky (1957). Hii ni kutokana na mikabala na nadharia ya wanaisimu wa mwanzo kushindwa kuonyesha uhusiano bayana uliokuwepo katika sentensi ambazo zinafanana. Kama mfano unaofuata chini unathibitisha.

Watoto wamekula wali

Wali umeliwa na watoto

Mawazo hayo ya Chomsky aliyoyatoa (1957) akapendekeza nadharia ambayo pamoja na kwamba nayo kwa kiasi kikubwa ilitumia taratibu za mkabala wa awali wa Sarufi Miundo Virai ilikwenda mbele na kuweka utaratibu wa kuhusisha aina hizo mbili. Chomsky ndipo alipoleta wazo la kuwepo kwa umbo ndani na umbo nje la sentensi. Kwa mujibu wa Chomsky sentensi zote hapo juu zinatokana na umbo ndani na kupata umbo nje kutoka umbo ndani kuna kanuni zinazotumika kuyageuza maumbo ndani, kanuni hizo zinajulikana kama kanuni za Ugeuzi (Massamba na wenzake 2003).

Kutokana na mkabala huu sentensi inayoelezea hali ya kutenda na ile inayoelezea hali ya kutendwa huwa zinaelezea muundo mmoja wa ndani. Chomsky (keshatajwa) aliitolea mifano dhana hii kwa kuuita muundo wa kwanza ndio muundo ndani ambao ni wenye kuleta maana ya msingi. Kwa upande wa muundo nje ndio unaoitwa muundo wa pili wenye kuleta maana zalishi.

Kazi iliyofanywa kuhusiana na uchambuzi wa viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba ni ile ya Maganga (keshatajwa) iliyolinganisha na kutofautisha kati ya lahaja za visiwani yaani Kiswahili sanifu, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba. Kazi hii ilijihusisha zaidi na vipengele vya kimofonolojia ikiachia mbali vipengele vingine hasa vya kimsamiati kuwepo mlingano wa maumbo na tofauti za kimaana, kuwepo mlingano wa maana katika maumbo tofauti kuwepo maumbo yanayolingana hali ya kutofautiana baadhi ya sauti, ambavyo mtafiti kwa maoni anahisi ni eneo muhimu na la kuvutia kufanyia uchunguzi.

Kutokana kuwa utafiti huu unachunguza viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Mgullu (1999) ameeleza vitenzi ni aina ya maneno ambayo hutumika katika sehemu muhimu sana ya kiarifu cha sentensi na ambayo huarifu / hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi.

Kihore na wenzake (2003) wanasema kuwa kitenzi ni aina ya neno inayotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Fasili hii ya Kihore inaungwa mkono nakusisitizwa na Habwe na Karanja (2004). Katika lugha ya Kiswahili vitenzi ni maneno pekee ambayo ni lazima yawepo katika sentensi ndipo sentensi iweze kuwa sentensi.

Kihore na wenzake (2003) wanasema kuwa kiambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Pia wanaeleza kuwa viambishi katika lugha ya Kiswahili huweza kujitokeza tu mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa vitenzi. Wanaeleza kuwa Kiswahili hakina viambishi kati.

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa vitenzi huitwa viambishi awali, ilhali vile ambavyo huwekwa katikati ya mzizi huitwa viambishi kati na vile ambavyo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa viambishi vifuatili. Ukweli ni kuwa Kiswahili hutumia viambishi vya aina mbili tu yaani viambishi awali na viambishi tamati.

Kutokana na kuwa njeo ni kategoria ya kisarafu ambayo huwakilisha muda au wakati tendo hufanyika (Tafsiri ya mtafiti). Njeo hueleza uhusiano ulioko baina ya wakati wa kutamka na wa kutenda. Njeo katika Kiswahili huelezwa na kitenzi.

Habwe na Karanja (2004) wakiinukuu Tuki (1990). Njeo katika lugha ya Kiswahili hutumika kwa maana ya wakati ambapo tendo lilitendeka au halikutendeka. Kiswahili kina njeo iliyopita, njeo iliyopo na njeo ijayo. Japokuwa kiambishi njeo ni kiambishi kinachowakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahsusi. Kila lugha ina mfumo wake wa kuwasilisha kiambishi cha aina hiyo. Katika lugha ya Kiswahili kiambishi hicho huwasilishwa na mofu maalumu inayojitokeza baada ya kiambishi nafsi.

Wataalamu mbali mbali kama Maganga, C. (1995), Habwe na Karanja (2004), Massamba na wenzake (2003) na Mgullu (1999) wameielezea dhana ya kiambishi njeo kwa majina tofauti tofauti. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (weshatajwa) kiambishi njeo ni mofu inayowakilisha mofimu ya wakati. Kwa upande mwingine Massamba na wenzake (washatajwa), wamekiita kiambishi hiki kuwa ni mofimu ya njeo. Naye Mgullu (keshatajwa) amekiita kiambishi hiki kwa jina hilo hilo. Wote kwa ujumla wamewafikiana kuwa: kiambishi njeo ni kiambishi awali kinachowakilisha wakati katika kitenzi.

Katika kazi hii kiambishi njeo kinatafsiriwa kuwa ni kijumbo kidogo au mofu iliyondani ya kitenzi inayowakilisha mofimu ya wakati. (Tafsiri ya mtafiti) Licha ya

viambishi njeo kupachikwa mwanzoni kabla ya mzizi wa kitenzi. Kitenzi cha Kiswahili pia huchukua mofimu ya njeo. Mofimu ya njeo pia ni kiambishi awali, kumaanisha kuwa mofimu hii huja kabla ya mzizi wa kitenzi (Habwe na Karanja weshatajwa).

Viambishi njeo katika lugha ya Kiswahili huambikwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. Kihore na wenzake (2003) wameorodhesha viambishi njeo katika Kiswahili kama inavyoonyeshwa hapo chini .

Jedwali 1.2: Viambishi njeo vya Kiswahili

Njeo	Mfano wa kiambishi	kitenzi	mtindo wa kitenzi
Wakati uliopo	-na-	- unase	kukubali
Wakati uliopo	-i-	hatulii	kukanusha
Wakati uliopita	-li-	alikulia	kukubali
Wakati uliopita	-ku-	hakulia	kukanusha
Wakati ujao	-ta-	atakuja	kukubali
Wakati uliopita hali timilifu	-me-	amerudi	kukubali
Hali ya mazoea	-hu-	humsaidia	kukubali

Baada ya kuona viambishi njeo mbali mbali kwa kupitia wataalamu mbalimbali viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba vimeundwa kwa irabu na konsonanti. Irabu katika lahaja ya Kipemba ni sawa sawa na irabu katika lugha ya Kiswahili. Irabu

hizo ni a, e, i, o na u. Tofauti ipo katika konsonanti, konsonanti katika lahaja ya Kipemba ni tofauti na za Kiswahili . Jadwali lililopo chini linathibitisha hilo.

Jedwali 1.3: Konsonanti na Viyeyusho katika Lahaja ya Kipemba

Matamshi		Mahali pa Kutamkia						
		Midom o	Midomo- - meno	men o	u fi zi	Kaaka a gumu	Kaaka a laini	korome o
VIPASUO	Ghuna	b			d		g	
	Visoghun a	p			t		k	
	Mpumuo	p ^h			t ^h		k ^h	
V I Z U I O KWAMIZI	Ghuna					j		
	Visoghun a					ĉ		
	Mpumuo					ĉ ^h		
VIKWAMIZI	Ghuna		V	δ	z		γ	h
	Visoghun a		F	θ	s	ʃ	x	
NAZALI		m			n	ɲ	ŋ	
VITAMBAZA					l			
VIMADENDE					r			
VIYEYUSHO		w				y		

Chanzo: Massamba na wenzake (2003)

1.9 Usuli wa Mada

Inasemekana kwamba maandiko ya mwanzo yaliyozungumzia kwa undani lugha ya Kiswahili ni yale ya Steere (1930) ambayo yalihusu sarufi ya lugha ya Kiswahili cha Unguja. Baada ya hapo kazi nyingi sana zinazohusiana na maendeleo ya Kiswahili ziliandikwa. Licha ya kazi hizo zilizoandikwa kuna nyingine zenye kuhusu viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba.

Habwe na Karanja (2004) wakiinukuu TUKI (1990) wameeleza njeo hutumika kwa maana ya wakati ambao tendo lilitendeka au halikutendeka. Njeo ni mofimu inayoambikwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi na inawakilisha wakati ambao tendo lilifanyika au lilifanywa (Tafsiri ya mtafiti). Kiswahili kina njeo iliyopita, njeo iliyopo na njeo ijayo. Kuna wataalamu mbali mbali ambao wamezungumzia kuhusu viambishi njeo. Mingoni mwa wataalamu hao ni Habwe na Karanja (2004) wameeleza kiambishi njeo ni kiambishi kinachowakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahsusi.

Massamba na wenzake (2003) wameeleza dhana ya kiambishi njeo ni mofimu ya wakati. Mgullu (1999) naye amelezea dhana ya kiambishi njeo kuwa ni mofimu inayowakilisha wakati. Kiambishi njeo ni kijiumbo kidogo au mofu iliyo ndani kitenzi inayowakilisha mofimu ya wakati (Tafsiri ya mtafiti). Viambishi njeo katika Kiswahili kwa mujibu wa Kihore na wenzake (2003) ni viambishi ambavyo huambikwa mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa kitenzi. Kuna wataalamu mbali mbali ambao wameeleza kuhusu viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba miongoni mwa wataalamu hao ni Salma (2011) katika kazi yake alibaini kuwa katika lahaja ya Kipemba kuna viambishi njeo vya njeo iliopo, njeo iliyopita, njeo ijao, hali timilifu, hali ya mazoea na hali ya kudadisi kwa tendo. Pia alibaini viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba ni tofauti na viambishi njeo vya Kiswahili sanifu. Kwa mfano kiambishi njeo cha njeo iliyopita katika Kiswahili sanifu ni –li- katika hali ya uyaakinishi na –ku- katika hali ya ukanushi wakati katika lahaja ya Kipemba ni –e-

katika hali zote mbili uyakinishi na ukanushi. Njeo ijao katika Kiswahili sanifu na katika lahaja ya Kipemba ni na Kiswahili sanifu ni –ta- katika hali zote (uyakinishi na ukanushi), kiambishi njeo cha wakati uliopo katika Kiswahili sanifu huwakilishwa na –na- na –a- katika lahaja ya Kipemba katika hali ya uyakinishi wakati z+(-i) ukanushi katika lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Kwa upande wa hali timilifu ni –na- katika uyakinishi na –ja- katika ukanushi, hali ya sharti ni –ki- katika uyakinishi na –sipo- katika ukanushi, hali ya kudadisi kwa tendo ni –enge- katika uyakinishi na –senge- katika ukanushi na hali ya kuendelea kwa tendo ni –ki- katika uyakinishi na hakuna kiambishi cha nje katika ukanushi.

1.10 Tatizo la Utafiti

Tafiti mbalimbali zimekwishafanywa kuchunguza viambishi njeo vya vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Wataalamu hao ni kama vile Salma (2011) na Maganga (1995) ingawa wamechunguza, tofauti za viambishi njeo na viambishi vya hali kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu, lakini hata hivyo hawakujihusisha na tofauti ya kanuni za kimofonolojia zinazotawala mabadiliko ya vitenzi vya Lahaja ya Kipemba. Kwa kiasi anachoelewa mtafiti, hakuna utafiti wa kina uliofanywa kwa madhumuni ya kubainisha michakato ya kimofonolojia miongoni mwa vitenzi vya lahaja ya Kipemba kuonesha miundo ndani na miundo nje, jambo ambalo linaweka pengo la kitaaluma. Kazi za Salma (keshatajwa) na Maganga (keshatajwa) zimetaja tu tofauti ya viambishi njeo kati ya Kipemba na Kiswahili sanifu bila kuweka wazi kanuni na michakato ya kifonolojia na kimofonolojia zinazojitokeza kuonesha

miundo ndani na miundo nje ya vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Kutokana na sababu hiyo, utafiti huu utachunguza viambishi njeo vya vitenzi vya lahaja ya Kipemba uchanganuzi wa kimofonolojia kuonesha muundo ndani na muundo nje.

1.11 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya aina mbili. Malengo hayo ni:

1.11.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchambua muundo wa vitenzi kuonesha namna viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba vinavyopitia kwenye mchakato wa kimofonolojia unaojitokeza kwenye muundo ndani na athari zake kwenye muundo nje.

1.11.2 Malengo Mahsusi

Ili kufikia lengo kuu la utafiti huu, mtafiti amechunguza madhumuni mahsusi yafuatayo:-

- a) Kubainisha viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba .
- b) Kueleza michakato ya kimofonolojia inayojitokeza katika miundo ndani kwenda miundo nje ya vitenzi vya lahaja ya Kipemba .
- c) Kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko yanayojitokeza kutoka muundo ndani kwenda muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba .

1.11.3 Maswali ya Utafiti

Kulingana na madhumuni ya utafiti yaliyotajwa hapo juu utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Vipi ni viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba ?
- b) Je, ni michakato ipi ya kimofonolojia inayojitokeza katika kubadilisha miundo ndani na miundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba ?
- c) Je, ni kanuni zipi za kifonolojia na kimofonolojia zinazotawala mabadiliko yanayotokea kutoka miundo ndani kwenda miundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba ?

1.12 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yataamsha ari kwa wasomi wa isimu kufanya tafiti nyingine zinazohusu maswali ya kiisimu yanayohusu viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba . Pia umeisaidia jamii kuelewa matumizi ya vimbishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba .Vile vile umeisaidia jamii kuelewa michkato ya kimofonolojia inayojitokeza kutoka miundo ndani na miundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Utaisaidia jamii kuelewa kanuni zinazotawala mabadiliko ya kimofonolojia kutoka miundo ndani na athari zake katika miundo nje. Itakuwa ni marejeo ya kimaktaba yatakayotumiwa na wasomi pamoja na watafiti wengine . Hata hivyo itakuwa ni sehemu ya marejeleo kwa walimu wa isimu na wanafunzi wao kwenye ngazi za sekondari, vyuo vya ualimu, taasisi zinazofundisha lugha na lughawiya na hata vyuo vikuu.

1.13 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba kuonesha michakato ya kimofonolojia inayojitokeza katika miundo ndani na miundo nje. Viambishi njeo vilivyochunguzwa ni viambishi njeo vinavyowakilisha wakati uliopo, wakati uliopita, wakati ujao, hali ya mazoea, hali timilifu na hali ya kudadisi jambo ambavyo vilipachikwa mwanzoni mwa mizizi ya vitenzi . Miongoni mwa vitenzi ambavyo vilipachikwa mwanzoni mwa vitenzi vilivyopachiwa viambishi hivyo njeo ni piga, cheza, imba, lia .Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Pemba katika Shehia ya Mtambwe Kaskazini katika kijiji cha Kele, Uondwe, Mpakanjia, Jambaji, Kiapaka na Chanjaani. Kwa hiyo vipengele vingine vya kifonolojia na kimofonolojia vinavyohusiana na alama, miundo ya silabi, uundaji wa maneno kutokana na silabi, vitamkwa na matamshi si vitu vitakavyoshughulikiwa. Vilevile hautojishughulisha na tofauti zitakazojitokeza kwenye fonolojia arudhi, kama shada na mikazo katika matamshi, toni na vipashio vingine vinavyohusiana na kipengele hiki cha fonolojia arudhi.

1.14 Changamoto za Utafiti huu na Suluhu Zake

Mtafiti alikutana na changamoto mbalimbali kabla na baada ya kwenda uwandani . Changamoto zilizojitokeza zilikuwa ni pamoja na upungufu wa fedha za utafiti ambazo zilihatajika kumsaidia mtafiti kununua vifaa na kufanya shughuli nyingine zinazohusu utafiti huu. Muda mfupi ambao mtafiti alipaswa kukamilisha utafiti

ambapo mtafiti alikuwa analazimika kuendeleza kikamilifu shughuli za kufundisha darasani na huku akiendelea na masomo yanayohusu utafiti huu. Pia tatizo jingine ni lile la baadhi watafitiwa kutokuwa na uelewa wa haraka sana katika kujaza dodoso walizopelekewa kutakana na umri wa watafitiwa ambao ulikua ni kuanzia miaka sitiini na kuendelea.

Aidha, mtafiti alikabiliana na tatizo la fedha kwa kujitahidi kubana matumizi kwa kuweka kifungu katika sehemu ya mshahara wake zilizomsadia kununua baadhi ya vifaa na kufanya shughuli nyingine za utafiti huu. Kuhusu tatizo la muda mtafiti alifanya bidii kubwa kwa kuongeza masaa ya kazi za kila siku ili kufidia muda. Kwa watafitiwa kushindwa kujaza dodoso kwa haraka sana mtafiti aliongeza kutumia mbinu ya usaili ambayo ilimrahisishia kukusanya data kwa haraka sana.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii inapasa kuzingatia maandiko mbali mbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Ili kuona ni namna gani wataalamu mbali mbali wamezungumzia kuhusu viambishi njeo katika lahaja ya Kipemba na kuangalia michakato ya kimofonolojia kwa kupia kanuni zinazotawala mabadiliko yanayotawala michakato ya kimofonolojia kutoka miundo ndani na miundo nje. Kwa mujibu wa Maganga (1995) ameandika juu ya mofonolojia ya lahaja za visiwani. Mazrui (1983) aliyefanya uchunguzi juu ya tofauti ya vipashio vya njeo za nyakati kati ya lahaja za Mvita Bajuni, Amu na Unguja, Hamad (2011) aliyefanya ulinganishi wa njeo na hali tofauti na wengineo.

Waliowahi kufanya kazi inayohusiana na mofu zinazowakilisha njeo za nyakati mbali mbali ni pamoja na Salma (2011). Katika kazi yake Salma alichunguza tofauti ya viambishi njeo na hali mbali mbali kati ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Aliangalia njeo za aina zote tatu; wakati uliopo, wakati, ujao na wakati uliopita. Pia aliangalia viambishi vinavyoakisi hali mbali mbali. Aligundua kwamba, viambishi njeo vya Kiswahili sanifu kwa kiasi kikubwa vinaachana na vile vya Kipemba. Habwe na Karanja (2004) wamegundua kuwa kiambishi njeo ni kiambishi

kinachowakilisha mofimu ya wakati katika lugha mahsusi na wamebaini kuna njeo ya iliyopo, njeo iliyopita na njeo iliyopo.

Massamba na wenzake (2003) wameona dhana ya kiambishi njeo ni mofimu ya wakati na wamegundua njeo zinazotumika katika lahaja ya Kipemba zinatofautiana na za Kiswahili sanifu. Kwa mfano katika lahaja ya Kipemba wanatumia -e – mfano wa neno epita wakati katika Kiswahili sanifu ni alipita kwa wakati uliopita Mgullu (1999) naye amegundua dhana ya kiambishi njeo kuwa ni mofimu inayowakilisha wakati na ameona kwa upande wake njeo iliopo, njeo iliopita na njeo ijao.

2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Muundo wa Vitenzi Vinavyozungumzia Viambishi Njeo

Baada ya uhuru, Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha ya Taifa, wataalamu mbalimbali wa lugha hawakuelekeza tena nguvu zao, katika kujishughulisha na tafiti zinazohusu viambishi njeo vya lahaja mbalimbali za Kiswahili. Maganga (1995) ameandika juu ya mofofonolojia ya lahaja za visiwani. Mazrui (1983) aliyefanya uchunguzi juu ya tofauti ya vipashio vya njeo za nyakati kati ya lahaja za Mvita Bajuni, Amu na Unguja, Hamad (2011) aliyefanya ulinganishi wa njeo na hali tofauti na wengineo.

Waliowahi kufanya kazi inayohusiana na mofu zinazowakilisha njeo za nyakati mbali mbali ni pamoja na Salma (2011). Katika kazi yake Salma alichunguza tofauti ya viambishi njeo na hali mbali mbali kati ya Kipemba na Kiswahili sanifu.

Aliangalia njeo za aina zote tatu; wakati uliopo, wakati, ujao na wakati uliopita. Pia aliangalia viambishi vinavyoakisi hali mbali mbali. Aligundua kwamba, viambishi njeo vya Kiswahili sanifu kwa kiasi kikubwa vinaachana na vile vya Kipemba. Mtafiti ameorodhesha tofauti ya viambishi njeo kati ya Kipemba na Kiswahili sanifu kama vilivyotajwa na Salma (2011), kwenye jedwali lifuatalo:-

Jedwali 2.1: Tofauti za Viambishi Njeo baina ya Kipemba na Kiswahili Sanifu

Kiambishi njeo cha wakati/hali	Kiswahili Sanifu		Kipemba	
Wakati uliopita	-li-	-ku-	-e-	-e-
Wakati timilifu	-me-	-ja-	n(a)	-ja-
Wakati ujao	-ta-	-ta-	-ta-	-ta-
Wakati uliopo	na	z+ (-i)	-a-	z+(-i)
Hali ya sharti	-ki-	-sipo-	-ki-	-sipo-
Hali ya kuendelea kwa tendo	-ki-	-	-ki-	-
Kudadisi kwa tendo	-nge-	-singe-	-enge-	-senge-

Kazi ya Salma (keshatajwa), imempa mwanga mtafiti wa kuona mwelekeo wa jinsi Kiswahili sanifu na lahaja zake zinavyoweza kulingana na kutofautiana, kwenye viambishi njeo vyake, ingawa haikutaja michakato ya kifonolojia na kimofonolojia iliyotawala mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje.

Maganga (1995), alifanya utafiti juu ya mofonolojia ya lahaja za visiwani alichunguza lahaja ya Kitumbatu, Kimakunduchi, Kipemba na Kiswahili sanifu. Licha ya kazi yake kuwa inahusu mofonolojia ya lahaja za visiwani kazi hii pia

inahusu kipengele cha viambishi njeo. Katika kipengele cha viambishi njeo aligundua kuwa kuna njeo iliyopita, njeo iliyopo, njeo ijao, hali timilifu, hali ya mazoea na hali ya kudadisi kwa tendo. Aligundua kuwa kuna tofauti kati ya viambishi njeo vya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Tofauti kati ya viambishi njeo kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi na Kiswahili sanifu kwa mujibu wa Maganga (keshatajwa), aligundua kiambishi njeo $\{z+TI\}$, kwa wakati uliopita yakinishi na kiambishi njeo $\{-e-\}$ kwa wakati uliopita kanushi. Kwenye njeo ya wakati timilifu yakinishi Kitumbatu na kimakunduchi hutumia kiambishi $-ma-$, ilhali kiambishi $\{-ja-\}$ hutumika kwa wakati uliopita kanushi kwenye lahaja mbili hizi. Kwenye wakati uliopo uyakinishi na ukanushi lahaja hizi hutumia kiambishi $\{-na-\}$. Wakati ujao kwenye hali zote mbili kwenye Kitumbatu na Kimakunduchi kiambishi $\{-ta-\}$ hutawala. Katika hali ya sharti na hali ya kuendelea kwa tendo Maganga (keshatajwa), aligundua kwamba kiambishi $\{-ka-\}$ hutumika kwenye Kipemba na Kimakunduchi. Kwenye Kipemba na Kiswahili sanifu. Maganga alionyesha viambishi njeo kama vilivyodokezwa kwenye jedwali la hapo juu. Massamba na wenzake (2003), walibainisha njeo za nyakati katika hali mbali mbali kwenye Kiswahili sanifu kama ilivyo kwenye jedwali lifuatalo:-

Jedwali 2.2: Njeo za Nyakati Mbali Mbali katika Kiswahili

Kiambishi njeo	Uyakinishi	Ukanushi
Wakati uliopo	-na-	$z^+ (-i)$
Wakati ujao	-ta-	ta
Wakati timilifu	-me-	ja
Wakati uliopita	-li-	-ku-

Hali ya sharti na kuendelea kwa tendo	-ki-	-
Hali ya kudadisi tendo	-nge	-singe
Hali ya kuwa kwa tendo	-li-	-si
Hali ya mfululizo wa matendo	-ka-	-

Kazi tangulizi zinazonekana katika utafiti huu zilikuwa mwongozo kwa mtafiti katika kuchunguza sarufi ya Kipemba na kubainisha watafiti jinsi wanavyoweza kuzibainisha njeo za nyakati mbali mbali na vipi Kiswahili sanifu kinavyojitenga na lahaja nyingine. Habwe na Karanja (2004) aliainisha njeo hizo hizo bila hitilafu.

2.3 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu (2004) ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Mekacha (2011) anaeleza nadharia kuwa ni mahitimisho yanayotokana na uchambuzi wa data ambao hujaribiwa na ubora wake ukithibitika hutumiwa kama mwongozo wa utafiti. Nadharia huundwa kutokana na uchambuzi na ufafanuzi wa data za kitakwimu (quantitative) au data stahilifu (qualitative) na kuzifanyia majumuisho na kisha mahitimisho ya kinadharia (Mekacha 2000).

Utafiti huu umetumia nadharia ya fonolojia zalishi . Nadharia ya fonolojia zalishi ni nadharia ambayo imeanzishwa na Chomsky (1957) na kutumiwa na wanaisimu wengi waliofanya kazi za isimu linganishi kama Maganga (keshatajwa) inadai kwamba matamshi ya kifonetiki pamoja na mofimu zilizojenga matamshi hayo kikawaida hujegwa kwa muundo ndani kwa upande mmoja na muundo nje kwa

upande mwingine. Mabadiliko yanayotokea kutoka muundo ndani hadi kufikia muundo nje hutawaliwa na kanuni moja au zaidi za kifonolojia na pale maumbo hayo yatakapokuwa yanalingana basi kunakuwa hakuna kanuni yoyote inayotawala. Kanuni hii hutupatia utabiri wa wazi unaohusu utamkaji wa muundo nje, mara tu baada ya kuutambua muundo ndani wa mofimu inayohusika. Pia ni rahisi kuitambua kanuni gani inahitajika kuubadili muundo ndani na kupata muundo nje

(a) Kanuni ya kifonolojia inayotawala muundo ndani, (b) mazingira ambapo kanuni ya kifonolojia inatumika, (c) mpangilio /kipaumbele wa matumizi ya kanuni moja kabla ya nyingine. Kanuni mbali mbali na michakato tofauti tofauti ya kifonolojia hujitokeza kutawala maumbo ya ndani na kusababisha maumbo ya nje ya aina tofauti kujitokeza.

Katika nadharia ya fonolojia zalishi mtafiti ameiteua kutokana na umuhimu mkubwa kwa mtafiti kuitumia kutokana na kuwa nadharia hii inahusu kanuni za kimofonolojia za miundo ya sentensi yaani miundo nje na miundo ndani na zitamsaidia katika kufikia malengo na matarajio yake.

Maganga (1995) alitumia nadharia hii katika kazi yake, pale alipobainisha kipengele cha kimofonolojia baina ya lahaja za Kitumbatu, Kiswahili sanifu, Kimakunduchi na Kipemba. Kwa kuwa mbinu hii ilimfikisha Maganga kwenye malengo yake na

kupata matukio yenye ufanisi mkubwa ndio maana mtafiti aliamini kwamba ingemsaidia katika kufikia malengo aliyokusudia.

2.4 Muhtsari wa Sura

Katika sura hii mtafiti ameelezea kuhusu mapitio ya kazi tangulizi aliyoyatumia mtafiti katika kufanyia utafiti wake, kiunzi cha nadharia alichokitua mtafiti katika utafiti huu. Mtafiti ni nadharia ya fonolojia zalisha ambayo inafanya kazi ya kubainisha viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba, kuelezea michakato ya kimofonolojia inayojitokeza kutoka muundo ndani na kuwa muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba na kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko ya kimofonolojia kutoka muundo ndani na kuweza kubadilika kuwa muundo nje katika viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba na kazi tangulizi za wataalamu mbali mbali zilizomsaidia mtafiti katika kuandika utafiti huu, kwa mfano kazi ya Salma ilichunguza kuhusu tofauti ya viambishi njeo kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu, Maganga alichunguza viambishi njeo katika lahaja ya Kitumbatu, Kimakunduchi, Kipemba na Kiswahili sanifu na aligundua uwiano wa moja kwa moja kati ya viambishi njeo katika lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi na alibaini lahaja hizi mbili zimeachana na Kipemba na Kiswahili sanifu. Kwa upande wa Massamba na wenzake (2003) walichunguza kuhusu njeo za nyakati mbali mbali na walibaini njeo za nyakati hizo zinajitenga katika lahaja ya Kitumbatu na njeo zilizoko katika Kiswahili sanifu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi.

Mbinu za utafiti zimeelezwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Katika sura hii mtafiti amebainisha taratibu, mbinu na njia mbalimbali zitazotumika katika ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti kuhusu muundo wa viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba kuonesha utaratibu wa mabadiliko ya muundo ndani kuwa muundo nje. Katika sura hii vimebainishwa vipengele kama vile muundo wa utafiti, eneo la utafiti, watoa taarifa, usampulishaji na vifaa vya utafiti. Pamoja na vipengele hivyo, vipengele vya ukusanyaji wa data, vyanzo vya data, mbinu za uchambuzi wa data na uwasilishaji wake umeongelewa kwenye sura hii.

3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa mchanganyiko ndio uliotumika katika ukusanyaji na uchambuzi data za utafiti huu. Kothari (2004) anaeleza kuwa, muundo wa utafiti ni mpangilio unaomuwezesha mtafiti utaratibu wa kukusanya na kuchambua data katika kiwango kizuri ambao pia unajumuisha upatikanaji wa data za uhakika zinazoendana na malengo ya utafiti. Mtafiti katika kazi yake hii ametumia muundo wa maelezo

kutokana na kuona ndio muundo unaofaa kulingana na kiwango cha watafitiwa aliowateua ambao ni wazee wa miaka sitiini na kuendelea.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Kisiwa cha Pemba, kwenye Shehia ya Mtambwe Kaskazini, katika vijiji vya Kele, Uondwe, Mpakanjia, Jambaji, Kiapaka na Chanjaani. Eneo hili lilichaguliwa kutokana na mtafiti kubaini kwamba kuna watumiaji wengi wa Kiswahili cha lahaja ya Kipemba ambayo itamsaidia kukusanya data zinazohusu viambishi njeo katika vitenzivya lahaja ya hiyo na kuweza kuchambua michakato ya kimofonolojia kuonesha miundo ndani na miundo nje ya vitenzi vya lahaja ya Kipemba pamoja na kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko ya kimofonolojia kutoka miundo ndani na miundo nje.

3.4 Watoa Taarifa

Walengwa wa utafiti huu ni wakaazi wa Mtambwe Kaskazini, kwa sababu hawa ni wazungumzaji asilia wa lahaja inayochunguzwa katika utafiti huu. Watafitiwa waliotoa taarifa ni watu wa makamo sitini wenye umri wa miaka sitini na kuendelea ambao waliteuliwa kiusampulishaji na mtafiti aliteua kwa kuwagawa kumi kutoka kila kijiji ambapo aliteua ishirini kutoka kila kijiji akagawa nambari moja mpaka ishirini na alimpatia kila mtafitiwa nambari yake. Kwa yoyote aliyebahatika na nambari moja mpaka kumi ndiye aliyemteua na akamtumia katika kukusanya data.

Kwa mujibu wa Kothari (2004) usampulishaji ni uteuzi wa kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwalo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake.

3.4.1 Sampuli na Usampulishaji

Usampulishaji ni mbinu yenye madhumuni maalumu na dhamira zinazohusisha uteuzi wa idadi ndogo ya wawakilishi wa walengwa wa utafiti unaofanywa na mtafiti kwa watafitiwa kwa madhumuni maalumu kutegemeana na taarifa zitakazohitajika kupatikana kwa ajili ya utafiti Kothari (2004). Suwed (2013), anaeleza uteuzi wa sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Katika utafiti huu isingekuwa rahisi kuwahusisha wazungumzaji na wataalamu wote wa Kiswahili. Zipo mbinu mbalimbali za kuchagua sampuli lakini uteuzi sampuli uliotumika katika utafiti huu ni mbinu ya sampuliji bahati nasibu ambapo mtafiti aliteua watu (wazee wa makamo) kumi kutoka kila kijiji na akagawa nambari moja hadi ishirini na alimgaia kila mmoja nambari moja kwa wale wote waliobahatika nambari moja mpaka kumi kwa kila kundi ndio aliowapa fursa ya kutafitiwa. Uteuzi huu ndio uliomsaidia mtafiti kupata watafiwa aliowataka kwa kuzingatia uwakilishi sawa wa makundi tofauti na kwa kuzingatia sababu mahsusni.

Suwed (keshatajwa) akiwanukuu Kombo na Tramp (2006) anasema, usampulishaji ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteuwa kundi la watu ambao anaamini

kuwa ni rasilimali anayoitegemea katika utafiti wake. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alitumia njia hii kwa kutoa fursa sawa kwa kila kundi aliloliteua mtafitiwa mmoja mwenye nambari sawa kwa lengo la kupata watafitiwa. Njia hii ilitumika kwa sababu ilimuwezesha mtafiti kuchagua wahojiwa kutokana na urahisi wao kufikiwa. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata sampuli ya watu wenye uzoefu wa kufahamu viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba (Kimtambwe) na kuangalia michakato ya kimofonolojia kuonesha miundo ndani na miundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba na kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko ya kimofonolojia kutoka miundo ndani na miundo nje hatimaye kupata data ambazo zimekuwa ni muhimili wa utafiti huu na kumsaidia mtafiti kufanya majumuisho mahsusi kulingana na lengo la utafiti. Mtafiti alichagua watoa taarifa kwa kutumia vigezo vya umri na ukaazi. Kwa mfano, alitumia wazawa na wale ambao wamekwishakaa kwa muda mrefu katika eneo la Mtambwe Kaskazini. Aidha alizingatia zaidi umri wa kuzaliwa na kuwagawa watu katika umri wao. Watu wazima katika eneo hilo hawajapata athari kubwa itokanayo na Kiswahili Sanifu. Data hizo ndizo zilizomsaidia mtafiti kuelewa viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Uchanganuzi wa kimofonolojia kuonesha muundo ndani na muundo nje.

3.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Utafiti huu ulitumia data za msingi ambazo zilipatikana kwa kutumia njia mbalimbali. Mbinu au njia za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti (Kothari 2004). Utafiti huu ulitumia mbinu za aina tatu ambazo ni mbinu ya dodoso, mbinu ya usaili na mbinu ya uchunguzi makini. Mtafiti amefikia

uamuzi wa kutumia mbinu za aina hiyo ili kupata uthabiti wa matokeo ya utafiti anaokusudia kuufanya. Mbinu alizotumia katika utafiti huu ni:-

3.5.1 Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (keshatajwa) dodoso ni mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadaye kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yameshajibiwa.

Adam na Kamuzora (2008), wanaeleza kuwa dodoso ni mbinu ya kukusanya data ambapo inahusisha maswali yaliyoandaliwa kuhusu mada fulani na kumtaka mtafitiwa kujibu kwa maandishi. Maswali haya yanaweza kuwa yanahitaji majibu mafupi au marefu kutegemena na taarifa inayohitajika pia na mtu anayepewa dodoso.

Walliman (2011) anaelezea kuwa maswali ya dodoso yako ya aina mbili. Aina ya kwanza ni ile inayohusisha maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jibu miongoni mwa majibu kadhaa yaliyopendekezwa. Aina hii ya dodoso ni rahisi kujibu na inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya dodoso ni ile inayohusisha maswali yasiyo funge ambayo hayatoi fursa kwa watafitiwa kuwa huru kueleza wanachokijua juu ya dhana fulani kutegemeana na kile kilichoulizwa. Aina hii haitoi uhuru kwa watafitiwa kueleza mawazo yao kwa ubainifu na uwazi na pia husaidia kupata taarifa nyingi zaidi.

Mbinu ya dodoso iliyotumika katika utafiti huu ilihusisha aina ya maswali funge . Mtafiti alitumia aina hii ya maswali ya dodoso katika utafiti wake kwa kuwapatia watafitiwa maswali ya aina hii kwa kuamini kuwa maswali ya aina hii ndio

yatakayopelekea majibu ya uhakika na umakini na kwa upande wa watafitiwa watakuwa huru na itawawezesha kuelezea kwa uhakika na ukweli bila ya woga wowote, mtafiti ameitumia mbinu ya dodoso kutokana na sababu ya kuona mbinu hii itaepusha usumbufu mkubwa kwa watafitiwa kutokana ndio maswali yanayoendana na watafitiwa kulingana na kiwango chao cha umri, hii ni kwa sababu dodoso ina umadhubuti na upungufu wake. Mtafiti ameona kwamba iwapo mbinu hii ilitumika ipasavyo itakuwa ni mbinu nzuri na ameitumia mtafiti kukusanya data za uhakika na kuweza kukamilisha utafiti kwa haraka sana. Vile vile ameona mbinu hii itamsaidia katika kukusanya data zake kwa muda mfupi ambazo zitampelekea kukamilisha utafiti wake kwa muda aliojiwekea. Pia itapelekea kuwatafiti watafitiwa aliowateua sawa sawa bila ya upendeleo wowote. Hata hivyo itampelekea mtafiti kupata taarifa nyingi kwa muda mfupi sana.

3.5.2 Uchunguzi Makini

Uchunguzi makini ni mbinu ya kukusanya data inayohusiana na kurikodi tabia za watu, vitu na matukio katika mpangilio maalumu kisayansi (Kothari 2004). Mbinu hii inachunguza vitu vyote vinavyotuzungumka. Uchunguzi makini ni wa aina mbili; uchunguzi makini unaodhibitiwa, huu hupatikana kwa kupitia vitu vilivyowekwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na uchunguzi makini usio na udhibiti, uchunguzi huu hupatikana katika sehemu za maumbile halisi na haupatikani kwa kutumia dhana za uchunguzaji bali hupatikana katika mazingira halisi yaani ya kimaumbile (Kothari 2004). Mtafiti alitumia mbinu hii ili kupata data za uhakika zilizoaminika na

kupunguza dosari kutokana njia ya uchunguzi makini ni njia ambayo mtafiti wa utafiti huu alitampatia data za awali na uhakika endapo atatumia uchunguzi makini wa udhibibiti na endapo hatatumia uchunguzi makini usio na udhibiti mtafiti hatopata data za awali za uhakika na umakini na dosari zitatokea kwa kukosa udhibiti wa wazungumzaji wa asili wa lahaja ya Kipemba . Kama anavyosema Walliman (keshatajwa) kuwa data za awali ni data zinazoaminika kwa sababu zimepatikana au kurekodiwa moja kwa moja kutoka kwenye tukio. Mtafiti katika utafiti huu alitumia uchunguzi makini wa kuweza kudhiti matukio kwa kwenda katika eneo la utafiti na akatafiti kwa kupitia watafitiwa halisi aliowateua ili kuweza kupata data za uhakika na kuepusha dosari kutokea.

3.5.3 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha mkusanyiko wa masuali kwa wasailiwa na kujibiwa ana kwa ana tu kwa wakati huo huo na mtafiti anarikodi katika daftari la kumbukumbu au katika tepu ya kurikodia. Kwa mujibu wa Kothari (2004) mbinu hii inamsaidia mtafiti kuweka bayana istilahi ambazo hazieleweki kwa watu walioulizwa pia mbinu hii humuwezesha mtafiti kupata taarifa za ziada na za kina. Kothari anaendelea kueleza kuwa mbinu hii inamruhusu mtafiti kuuliza masuali ya ziada na pia kumuwezesha kuwa karibu na watoa taarifa.

Walliman (keshatajwa) amegawa mbinu ya usaili katika aina tatu ambazo ni usaili wa ana kwa ana, usaili wa kikundi na usaili wa kutumia simu (mtandao). Ingawa mbinu hii inaweza kufanywa kwa njia zote hizo, katika utafiti huu, mtafiti aliitumia

mbinu hii kwa kuwasaili watafitiwa wake wa data za lahaja ya Kipemba kwa kutumia maswali wazi ambayo hayakufungwa hata kidogo akayagawa kwa watafitiwa wake na akawafanyia usaili wa ana kwa ana kwa lengo la kupata data za uhakika.

Aidha, mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu kadhaa, kwanza, ni kwa ajili ya kupata uthabiti wa majibu ya watafitiwa. Pili, ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli yake kwa wepesi na kwa usahihi zaidi. Hii imewezekana kwa sababu mtafiti alipata fursa na wahojiwa ana kwa ana na kuwauliza maswali na kurikodi majibu yao papo kwa papo wakati mahojiano yao yanaendelea. Pia maswali ambayo yalikosa majibu aliweza kuyatafutia ufumbuzi papo kwa papo. Tatu, ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi, kwasababu watafitiwa waliweza kuuliza maswali na mtafiti alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali ya ziada fursa ambayo isingepatikana katika mbinu nyingine za kukusanyia data kama vile usaili na nyinginezo.

3.6 Mbinu za Kuchambua na Kufafanua Data

Kwa mujibu wa Jamal na Kamuzora (2008) wakimnukuu Kothari (2004), uchambuzi wa data ni mchakato wa kuchanganua taarifa fulani zilizopo ili kupata mpangilio wa mahusiano miongoni mwa makundi mbalimbali ya taarifa zilizokusanywa. Data katika utafiti huchambuliwa na kufafanuliwa kwa kutumia mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kimaelezo na mkabala wa kitakwimu. Kwa mujibu wa Walliman (keshatajwa) mkabala wa kiidadi (kitakwimu) ni mbinu ya kuchambua na kufafanua

data kwa kutumia namba ili kurekodi taarifa na kuwasilisha kwa kutumia mbinu za kitakwimu.

Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi (kimaelezo) ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Katika utafiti huu mtafiti alijikita zaidi kwenye uchambuzi unaozingatia mkabala usio wa kiidadi (kimaelezo). Mtafiti alijishughulisha na maswali ya lugha na lugha inahitaji usahihi wa vipashio vitumikavyo kujenga lugha hiyo, bila kuzingatia sana wingi au uchache wa idadi ya wazungumzaji. Kwa hivyo njia ya uchambuzi wa kimaelezo inaonekana kufaa zaidi kuliko ule wa kiidadi. Kutokana na sababu hiyo mtafiti alitumia mkabala usio wa kiidadi kufafanua na kuchambua data kwa pale alipolazimika kufanya hivyo.

3.7 Misingi ya Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Mathooko na wenzake (2007:15) misingi ya maadili ya utafiti ni kaida zinazoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu. Katika utafiti huu maadili ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotangamana nao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Kwa vile utafiti huu ulihusisha watu na asasi mbalimbali, na kwa sababu kila asasi ina sheria, taratibu, kanuni na utamaduni wake. Kwa hiyo mtafiti alihitaji kupata kibali ambacho kilimsaidia kuingia katika maeneo husika.

Suala jingine la kimaadili ambalo mtafiti alilingatia ni kuwaomba washiriki kushiriki kwa hiari na kujitolea katika kutoa data. Schutt (2006) anasema kuwa, kwa watafiti, ni jambo la muhimu sana kuhakikisha kwamba washiriki wa utafiti wanashiriki kwa kujitolea. Hivyo basi, wakati wa kutoa maelezo tangulizi ya mwongozo wa maswali ya usaili na dodoso mtafiti aliweka bayana malengo ya utafiti huu na aliwaomba watafitiwa wajitolee wakiwa huru na kushiriki kikamilifu katika usaili na kujibu maswali yaliyokuwepo katika dodoso na usaili. Pia mtafiti alilingatia suala la usiri wakati wa kukusanya data kiasi kwamba hakuna mtu mwingine zaidi ya mtafiti aliyejua chanzo cha data hizo na wala haukubainishwa utambulisho wa mshiriki ama mhojiwa.

Washiriki hawakutakiwa kuandika majina yao ili kulinda siri ya mtoa data. Kulingana na ahadi ambayo mtafiti aliitoa kwa wahojiwa wake, data zote alizokusanya mtafiti kwa kutumia mbinu ya usaili, dodoso na uchunguzi makini uwandani taarifaalizopata mtafiti alizitunza kwa usiri mkubwa. Hii inaonyesha kwamba mtafiti alichukua hatua muhimu katika kuzingatia vipengele vyote vya uzingativu wa maadili katika utafiti huu.

Mtafiti alifanya kila awezavyo kuhakikisha usalama wa watafitiwa wake, aliwataka watafitiwa kuwa huru na wasiwe na hofu ya kujieleza. Pia aliwadokeza mwanzo

watafitiwa wake kwamba taarifa atakazozipata kutoka kwao ni siri baina yake na watafitiwa wake tu.

3.8 Muhtasari wa Sura

Sura hii mtafiti amebainisha mbinu alizotumia katika ukusanyaji wa data ambazo ni mbinu ya dodoso, usaili na uchunguzi makini, muundo wa utafiti, ukusanyaji na uchambuzi wa data, uwiano wa viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba ili kubainisha muundo ndani na muundo nje, eneo la utafiti ambalo ni Mtambwe Kaskazini katika kijiji cha Uondwe, Kele, Jambaji, Chanjaani, Mpakanjia na Kiapaka, watoa taarifa ambao ni watu sitini ambapo mtafiti aliteua kumi kutoka kila kijiji wenye umri kati ya miaka sitiini na kuendelea kwa kutumia usampulishaji bahati na sibu pamoja na misingi ya utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UFAFANUZI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili data za utafiti. Data zinawasilishwa na kujadiliwa kulingana na malengo mahsusi ya utafiti ambayo ni kubainisha viambishi njeo vya vitenzi vya lahaja ya Kipemba kuonesha muundo ndani na muundo nje, kubainisha michakato ya kimofonolojia inayojitokeza katika miundo ndani na miundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba na kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba.

4.2 Viambishi Njeo Katika Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba

Katika sehemu hii yanaelezwa maumbo ya njeo za wakati zinazotumika katika lahaja ya Kipemba . Kwa mujibu wa data lahaja ya Kipemba ina viambishi njeo kama kiambishi njeo kinachoonesha wakati uliopo, hali timilifu , wakati uliopita , wakati ujao, wakati wa mazoea na wakati wa kudadisi tendo . Uainishaji huu utazingatia hali ya uyaakinishi na hali ya ukanushi. Jedwali na. 6: Linaonesha Mifano ya viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba .

Jedwali 4.1: Mifano ya Viambishi Njeo katika Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba

Nyakati	Lahaja ya Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu	
	uyakinishi	ukanushi	uyakinishi	ukanushi
Wakati uliopo	nacheza twacheza	sichezi hatuchezi	ninacheza tunacheza	sichezi hatuchezi
	wacheza mwacheza	hawachezi hamuchezi	unacheza munacheza	huchezi hamuchezi
	acheza wacheza	hachezi hawachezi	anacheza wanacheza	hachezi hawachezi
Wakati uliopita	necheza twecheza	secheza hatwecheza	nilicheza tulicheza	sikucheza hatukucheza
	echeza wecheza	hecheza hewecheza	alicheza walicheza	hakucheza hawakucheza
	echeza wecheza	hecheza hawecheza	alicheza walicheza	hakucheza hawakucheza
Wakati ujao	ntacheza tutacheza	sitacheza hatuchezi	nitacheza tutacheza	sitacheza hatucheza
	utacheza mtacheza	hutacheza hamuchezi	utacheza mutacheza	hutacheza hamutacheza
	atacheza watacheza	hachezi hawachezi	atacheza watacheza	hatacheza hawatacheza
Wakati timilifu	nnacheza tunacheza	sichezi hatuchezi	nimecheza tumecheza	Sikucheza hatukucheza
	unacheza mnacheza	huchezi hamchezi	umecheza mumecheza	huchezi hamuchezi
	anacheza wanacheza	hachezi hawachezi	amecheza wamecheza	hakucheza hawachezi
Hali ya mazoea	nacheza twacheza	sichezi hatuchezi	ninacheza tunacheza	sichezi wamecheza
	wacheza mwacheza	hawachezi hamuchezi	wanacheza munacheza	hawachezi hamuchezi
	acheza wacheza	hachezi hawachezi	anacheza wanacheza	hachezi hawachezi

Hali ya kudadisi tendo	nengecheza twengecheza	nesengecheza tusengecheza	nengecheza twengecheza	nisingecheza tusingecheza
	wengecheza mwengecheza	wesengecheza musengecheza	wengecheza mwengecheza	wasingecheza musingecheza
	engecheza wengecheza	esengecheza wesengecheza	engecheza wengecheza	esingecheza wasisengecheza

Chanzo : Data ya uwandani (2015)

Data katika jedwali la hapo juu inaonyesha mifano mbalimbali ya njeo za wakati zinazotumika katika lahaja ya Kipemba. Njeo zilizoonyeshwa ni za wakati uliopo, wakati timilifu, wakati uliopita, wakati ujao, wakati wa mazoea na wakati wa kudadisi tendo katika nafsi ya kwanza umoja na uwingi, nafsi ya pili umoja na uwingi na nafsi ya tatu umoja na uwingi katika hali ya uyakinishi.

4.2.1 Kiambishi Njeo cha Wakati Uliopo katika Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba

Kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba kwenye hali ya uyakinishi ni $\{-a-\}$ na katika hali ya ukanushi ni $\{z+-i\}$. Ili kuthibitisha hayo mtafiti ameonesha maumbo ya vitenzi vinavyoonesha njeo ya wakati uliopo kwa lahaja ya Kipemba. Angalia jedwali na.(1) linaonyesha hali ya uyakinishi na jedwali Na. (2) kwa hali ya ukanushi.

Jedwali 4.2. Kiambishi kinachowakilisha Njeo ya Wakati Uliopo (Uyakinishi)

Kitenzi	Nafsi	Kitenzi cha L/Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
Kitenzi	Nafsi	M/ndani	M/nje	
piga	N1- umoja	ni- <i>a</i> -piga	napiga	ninapiga
	N1-uwingi	tu- <i>a</i> -piga	twapiga	tunapiga
	N2-umoja	u- <i>a</i> -piga	wapiga	unapiga
	N2-uwingi	mu- <i>a</i> -piga	mwapiga	munapiga
	N3-umoja	a- <i>a</i> -piga	apiga	anapiga
	N3-uwingi	wa- <i>a</i> -piga	wapiga	wanapiga
imba	N1- umoja	ni- <i>a</i> -imba	naimba	ninaimba
	N1-uwingi	tu- <i>a</i> -imba	twaimba	tunaimba
	N2-umoja	u- <i>a</i> -imba	waimba	unaimba
	N2-uwingi	mu- <i>a</i> -imba	mwaimba	munaimba
	N3-umoja	a- <i>a</i> -imba	aimba	anaimba
	N3-uwingi	wa- <i>a</i> -imba	waimba	wanaimba
-fa-	N1- umoja	ni- <i>a</i> -fa	nafa	ninakufa
	N1-uwingi	tu- <i>a</i> -fa	twafa	tunakufa
	N2-umoja	u- <i>a</i> -fa	wafa	unakufa
	N2-uwingi	mu- <i>a</i> -fa	mwafa	munakufa
	N3-umoja	a- <i>a</i> -fa	afa	wanakufa
	N3-uwingi	wa- <i>a</i> -fa	wafa	wanakufa
-lia	N1- u m o j a	a- <i>a</i> -lia	alia	analia
	N1-uwingi	tu- <i>a</i> -lia	twalia	tunalia
	N2-umoja	u- <i>a</i> -lia	walia	unalia
	N2-uwingi	mu- <i>a</i> -lia	mwalia	munalia
	N3-umoja	a- <i>a</i> -lia	alia	analia
	N3-uwingi	wa- <i>a</i> -lia	walia	wanalia

Chanzo: Data ya uwandani (2015)

Katika jedwali la hapo juu linaonyesha kwa namna gani Kipemba kinatumia kiambishi (-a-) kubainisha njeo ya wakati uliopo katika hali ya uyakinishi.

Jedwali 4.3: Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Wakati Uliopo (Ukanushi)

Kitenzi	Nafsi	Kitenzi cha L/Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
		M/ndani	M/nje	
piga	N1- umoja	si-pigi	sipigi	sipigi
	N1-uwingi	ha-tu-pigi	ha-tu-pigi	ha-tu-pigi
	N2-umoja	ha-u-pigi	hupigi	haupigi/hupigi
	N2-uwingi	ha-mu- pigi	hamupigi	hamupigi
	N3-umoja	ha-pigi	hapigi	hapigi
	N3-uwingi	ha-wa-pigi	hawapigi	hawapigi
imba	N1- umoja	si-imbi	siimbi	siimbi
	N1-uwingi	ha-tu-imbi	hatuimbi	hatuimbi
	N2-umoja	ha-u-imbi	huimbi	huimbi
	N2-uwingi	ha-muimbi	hamuimbi	hamuimbi
	N3-umoja	ha-imbi	haimbi	haimbi
	N3-uwingi	ha-wa-imbi	hawaimbi	hawaimbi
-fa-	N1- umoja	si-fi	sifi	sifi
	N1-uwingi	ha-tu-fi	hatufi	hatufi
	N2-umoja	ha-u-fi	hufi	hufi
	N2-uwingi	ha-mu-fi	hamufi	hamufi
	N3-umoja	ha-a-fi	hafi	hawafi
	N3-uwingi	Ha-wa-fi	hawafi	hawafi
-lia-	N1- umoja	si-lii	silii	silii
	N1-uwingi	ha-tu-lii	hatulii	hatulii
	N2-umoja	ha-u-lii	hulii	hulii
	N2-uwingi	ha-mu-lii	hamulii	hamulii
	N3-umoja	ha-lii	halii	halii
	N3-uwingi	ha-wa-lii	hawalii	hawalii

Chanzo: Data ya uwandani (2015)

Kwa ujumla data zinaonesha kwamba, Kipemba hutumia kiambishi $\{-a-\}$ katika hali ya uyaikinishi na $\{z+ -i\}$ kwenye hali ya ukanushi. Athari za kimabadiliko kwenye miundo ndani kuelekea miundo nje imejitokeza kwenye hali ya uyaikinishi tu kwenye lahaja ya Kipemba kupitia michakato na kanuni fulani fulani kama itakavyoonyeshwa kwenye lengo la pili na la tatu la utafiti huu.

4.2.2 Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Hali Timilifu

Kiambishi kinachowakilisha mofu ya njeo ya wakati timilifu (wakati uliopita kitambo kifupi), kwenye hali ya uyaikinishi katika lahaja ya Kipemba ni $\{-n(a)-\}$. Data katika jedwali na.(3) iliyopo hapo chini inatoa ushahidi juu matumizi ya kiambishi $n(a)$ katika Kipemba (Kimtabwe) kuonyesha njeo ya wakati timilifu katika lahaja ya Kipemba kwenye uyaikinishi. Kwa upande wa hali ya ukanushi, lahaja ya Kipemba hutumia kiambishi $\{-ja-\}$ kuwakilisha njeo ya wakati timilifu. Data katika jadweli Na.7, inatoa ushahidi juu ya matumizi ya kiambishi $\{-ja-\}$ katika Kipemba (Kimtabwe) na kuonyesha njeo katika kitenzi timilifu katika lahaja hii hali ya ukanushi.

Jedwali 4.4: Kiambishi cha Wakati Timilifu Kuwakilisha Njeo Uyaikinishi na Ukanushi

Matumizi ya kiambishi $n(a)$ katika wakati timilifu (yakinishi)	Matumizi ya kiambishi ja katika wakati timilifu (ukanushi)	Tafsiri kwa Kiswahili sanifu (uyakinishi)	Tafsiri kwa kiswahili sanifu (ukanushi)
$nn-(a)$ soma	$sijasoma$	nimesoma	sijasoma
$tun-(a)$ soma	$hatujasoma$	tumesoma	hatujasoma
$kun-(a)$ soma	$hujasoma$	umesoma	hujasoma

mun-(a)soma	hamujasoma	mumesoma	hamujasoma
kan-(a)soma	hajasoma	amesoma	hajasoma
wan-(a)soma	hawajasoma	wamesoma	hawajasoma

Chanzo: Data ya Uwandani(2015)

Kwa ujumla lahaja ya Kipemba hutumia kiambishi (n-(a) kuwakilisha njeo ya wakati timilifu, kuwakilisha njeo ya wakati huo katika hali yakinishi. Hata hivyo kwa upande mwingine lahaja ya Kipemba hutumia kiambishi (-ja-) kuwakilisha njeo ya wakati timilifu kwenye hali ya ukanushi.

4.2.3 Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Wakati Uliopita

Mofu au kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopita kwenye lahaja ya Kipemba, katika hali ya uyaakinishi na ukanushi ni {-e-}. Jedwali Na.(7) na jedwali Na. (8) hapo chini yanaonyesha kwa uwazi hoja zilizoainishwa na mtafiti.

Jedwali 4.5: Njeo za Wakati Uliopita katika Hali ya Uyaakinishi

Kitenzi	Nafsi	Lahaja ya Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
		M/ndani	M/nje	
piga	N1- umoja	ni-e-piga	nepiga	nilipiga
	N1-uwingi	tu-e-piga	twepiga	tulipiga
	N2-umoja	u-e-piga	wepiga	ulipiga
	N2-uwingi	mu-e-piga	mwepiga	mulipiga
	N3-umoja	a-e-piga	epiga	alipiga
	N3-uwingi	wa-e-piga	wepiga	walipiga

Chanzo: Data ya Uwandani: (2015)

Katika jedwali Na. (7) hapo juu inaonesha kuwa kwenye lahaja ya Kipemba, kiambishi {-e-} ndicho kinachowakilisha njeo ya wakati uliopita, hali ya uyakinishi katika lahaja ya Kipemba. Kiambishi hicho kimejidhihirisha wazi kwenye muundo wa nje. Hata hivyo kwa kuwa kiambishi hiki kina muundo wa irabu, kimejikuta kinayaathiri maumbo ya nje ya vitenzi kupitia michakato mbalimbali ya kifonolojia kwa kutumia kanuni kadhaa kama mtafiti atakavyobainisha kwa uwazi kwenye lengo la pili na la tatu kwenye tasnifu hii.

Jedwali 4.6: Kiambishi Njeo cha Wakati Uliopita (Hali ya Ukanushi)

Kitenzi	Nafsi	Lahaja ya Kipemba		Maelezo Kiswahili Sanifu
		M/ndani	M/nje	
piga	N1- umoja	si-e-piga	sepiga	<i>sikupiga</i>
	N1-uwingi	ha-tu-e-piga	hatwepiga	<i>hatukupiga</i>
	N2-umoja	ha-u-e-piga	hwepiga	<i>hukupiga</i>
	N2-uwingi	ha-mu-e-pig a	hamwepiga	<i>hamukupiga</i>
	N3-umoja	ha-a-e-piga	hepiga	<i>hakupiga</i>
	N3-uwing i	ha-wa-e-pig a	hawepiga	<i>hawakupiga</i>

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Katika jedwali lililopo hapo juu kiambishi {-e-} chenye muundo wa irabu inayowakilisha njeo ya wakati uliopita ukanushi na pia kwa muundo wake kimeleta athari kubwa kwenye muundo wa nje kupitia kanuni na michakato mbalimbali kama itakavyoelezwa kwenye lengo la pili na la tatu la kazi hii. Kwa ujumla wake

kiambishi njeo kinachowakilisha wakati uliopita katika Kipemba ni *{-e-}* Katika hali ya ukanushi.

4.2.4 Kiambishi Njeo cha Wakati Ujao

Katika Kipemba, kiambishi kitumikacho kuwakilisha njeo ya wakati ujao katika hali ya uya kinishi kwenye kitenzi cha kawaida ni *{-ta-}*. Kupitia kiambishi hiki katika hali ya uya kinishi na ukanushi hakuna mabadiliko yoyote yanayojitokeza kutoka muundo wa ndani kwenda muundo wa nje kwenye lahaja ya Kipemba. Jedwali Na. (8) linaonyesha ithibati juu ya haya yaliyobainishwa na mtafiti.

Jedwali 4.7: Kiambishi kinachowakilisha Njeo ya Wakati Ujao Ukanushi

Kitenzi	Nafsi	Kitenzi cha Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
		M/ndani	M/nje	
piga	N1- umoja	si-ta-piga	sitapiga	sitopiga
	N1-uwingi	ha-tu-ta-piga	hatutapiga	hatutopiga
	N2-umoja	hu-ta-piga	hutapiga	hutopiga
	N2-uwingi	ha- mu-ta-piga	hamutapiga	hamtopiga
	N3-umoja	ha-ta-piga	hatapiga	hatopiga
	N3-uwingi	ha-wa-ta-piga	hawatapiga	hawatopiga

Chanzo: Uwandani (2015)

4.2.5 Kiambishi Kinachowakilisha Hali ya Kudadisi kwa Tendo

Kiambishi kinachowakilisha mofu ya hali ya kudadisi tendo, katika lahaja ya Kipemba ni *-enge*, *- engali* na *-engeli* kwenye hali ya uya kinishi na *-senge*, *-sengali*,

-sengeli, kwa upande wa hali ya ukanushi. Maumbo ya vitenzi vya Kipemba yaliyoambikwa viambishi vya hali ya kudadisi tendo (***-enge***) kwenye uyakinishi na mofu ya ukanushi (***-senge***) kwa Kipemba hujitokeza kama ilivyo katika data iliyomo kwenye jedwali Na: (13)

Jedwali 4.8: Kiambishi Kinachowakilisha Hali ya Kudadisi kwa Tendo katika Kipemba

Kitenzi	Nafsi	Lahaja ya Kipemba			Maelezo Kiswahili sanifu	
		Uyakinishi		Ukanushi	Uyakinishi	Ukanishi
		M/Ndani	M/Nje			
piga	N 1 - umoja	Ni- <i>e-ngepiga</i>	<i>nengepiga</i>	<i>nisengepiga</i>	<i>ningepiga</i>	<i>nisingepiga</i>
	N1-uw ingi	Tu- <i>e-ngepiga</i>	<i>twengepiga</i>	<i>tusengepiga</i>	<i>tungepiga</i>	<i>tusingepiga</i>
	N 2 - umoja	<i>uengepiga</i>	<i>wengepiga</i>	<i>usengepiga</i>	<i>ungepiga</i>	<i>usingepiga</i>
	N2-uw ingi	<i>muengepiga</i>	<i>mwengepiga</i>	<i>musengepiga</i>	<i>mungepiga</i>	<i>musingepiga</i>
	N 3 - umoja	<i>aengepiga</i>	<i>engepiga</i>	<i>asengepiga</i>	<i>angepiga</i>	<i>asingepiga</i>
	N3-uw ingi	<i>waengepiga</i>	<i>wengepiga</i>	<i>wasengepiga</i>	<i>wangepiga</i>	<i>wasingepiga</i>

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Kwa mujibu wa data katika jedwali na.13 hapo juu kwenye lahaja ya Kipemba viambishi vinavyowakilisha hali ya kudadisi kwa tendo kwenye hali ya uyakinishi na ukanushi vina athari kubwa na vinayageuza maumbo ya ndani na kujenga maumbo mapya ya nje, kupitia kanuni mbali mbali kama itakavyojitokeza kwenye lengo la pili na la tatu. Kwa ujumla kiambishi kinachowakilisha hali ya kudadisi kwa tendo

kwenye lahaja ya Kipemba ni *-nge*, *-ngali* na *-ngeli* kwenye uyaikinishi na *-singe*, *-singali*, *-singeli* kwenye ukanushi.

4.2.6 Kiambishi cha Hali ya Mazoea

Kama ilivyo katika njeo ya wakati uliopo, Kipemba katika hali ya mazoea hutumia kiambishi $\{-a-\}$ kwenye uyaikinishi na $\{z+ -i\}$ kwenye ukanushi. Katika hali hii, kwenye Kipemba kitenzi hujitokeza kama ilivyo kwenye uwakilishi wa wakati uliopo kwenye lahaja hiyo. Tuangalie data ifuatayo kuthibitisha yale yaliyobainishwa na mtafiti hapo juu.

Jedwali 4.9: Kiambishi cha Hali ya Mazoea

Kitenzi	Nafsi	Kitenzi cha Lahaja ya Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
		M/Ndani	M/Nje	
aja	N-1 umoja	ni-a-ja	naja	ninakuja
	N-1 uwingi	tu-a-ja	twaja	tunakuja
feli	N-2 umoja	u-a-feli	wafeli	unafeli
	N-2 uwingi	mu-a-feli	mwafeli	munafeli
fika	N-3 umoja	a-a-fika	afika	anafika
	N-3 uwingi	wa-a-fika	wafika	wanafika

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Data hiyo inabainisha kuwa katika lahaja ya Kipemba katika hali ya mazoea hutumia kiambishi *-a-* kuonesha uyaikinishi kama katika kitenzi *aja* tunapa neno

ni-a-ja katika muundo ndani na neno *naja* katika muundo nje kwa nafsi ya kwanza umoja.

Kwa ujumla, kama inavyoonekana katika data ya hapo juu tunaweza kusema kwamba kiambishi kinachowakilisha hali ya mazowea kwenye uyakinishi ni $\{-a-\}$ na kwenye ukanushi ni $z+(-i)$.

4.3 Michakato Ya Kimofonolojia Kwenye Viambishi Njeo

Sehemu hii inaangazia michakato ya kimofonolojia inayotawala mabadiliko kutoka miundo ndani na kuwa miundo nje katika viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba.

Kama ilivyooneshwa kwenye majadwali na . 1-7, lahaja ya Kipemba ina viambishi njeo vinavyowakilisha nyakati mbali mbali. Viambishi hivi ndivyo vinavyoathiriana na viambishi nafsi kuigeuza miundo ndani katika vitenzi na kujenga miundo mipya ya vitenzi.

Data iliyowasilishwa kwenye jedwali Na. 1, inaonesha kuwa iwapo kiambishi awali cha nafsi ya kwanza umoja kitafuatiwa na kiambishi cha njeo ya wakati uliopita katika lahaja ya Kipemba, panatokea udondoshaji. Udondoshaji huo unatokea kwenye mpaka wa mofu mbili; mofu $\{ni-\}$ inayowakilisha nafsi ya kwanza umoja na mofu $\{-e-\}$ inayowakilisha njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha uyakinishi cha Kipemba. Irabu ya juu mbele / *i* /, ambayo ni irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja inadondoka na irabu ya kati mbele / *e* /, ambayo inawakilisha mofu ya njeo ya wakati uliopita katika lahaja ya Kipemba

inatawala. Kutokana na hali hii, muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba yanayowakilisha wakati uliopita kwa nafsi ya kwanza umoja yakinishi yanakuwa na sura kama *nepiga*, *necheka*, *nesoma*, *nenuna* n.k. Kanuni kuu iliyotawala kuubadilisha muundo wa ndani na kuleta muundo wa nje ni kanuni ya udondoshaji. Kanuni hii tunaweza kuiwasilisha kama:-

/ i / [ϕ] / - / é / .

Ufafanuzi zaidi kuhusiana na kanuni hii umewekwa wazi kwenye lengo la tatu la kazi hii ni kuwa irabu / i / katika mazingira na kufuatiliwa na / e / kwa hiyo irabu / i / hudondoka na kubaki /e / kama mfano hapo juu unavyoonesha.

Jedwali 4.10: Vitenzi Vinavyoonyesha Njeo ya Wakati Yakinishi Uliopita kwa Nafsi ya Kwanza Umoja

Nafsi	Lahaja ya Kipemba	Maelezo Kiswahili sanifu
N 1 Umoja	Nesoma kucha wala sefaulu ntihani	Nilisoma kucha wala sikufaulu mtihani.
	Necheka ta nposikia yule nchawi ekufa.	Nilicheka hata niliposikia yule mchawi alikufa
	Nepiga usingizi mpaka ausubuhi	Nilipiga usingizi mpaka asubuhi.
	Nami ni ntu, nenuna	Nmi ni mtu, nilinuna

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Kanuni ya udondoshaji pia imejitokeza pale ambapo kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya tatu umoja au uwingi kitafatiwa na kiambishi cha njeo ya wakati uliopita $\{e\}$. Udondoshaji huu nao pia umejitokeza kwenye mpaka wa mofu mbili; mofu $\{a\}$, inayowakilisha nafsi ya tatu umoja na mofu $\{-e\}$ inayowakilisha njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha Kipemba. Irabu ya chini $/a/$ ambayo ni kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya tatu umoja inadondoka na irabu ya kati mbele $/e/$ ambayo inawakilisha mofu ya njeo ya wakati uliopita katika lahaja ya Kipemba inatawala. Vile vile kiambishi awali $/wa/$, kinachowakilisha nafsi ya tatu uwingi kinapokutana na irabu ya kati mbele $/e/$ ambayo inawakilisha mofu ya njeo ya wakati uliopita katika lahaja ya Kipemba udondoshaji hutokea. Kinachodondoka hapa ni irabu ya chini $/a/$ ambayo kwa hapa ni irabu ya kiambishi awali nafsi ya tatu uwingi. Kutokana na hali hii, maumbo ya vitenzi vya Kipemba yanayowakilisha wakati uliopita kwa nafsi ya tatu yanakuwa na sura kama *epiga, echeka, esoma, enuna* kwa nafsi ya tatu umoja na *wepiga, wecheka, wesoma, wenuna* kwa nafsi ya tatu uwingi. Kanuni iliyotawala mabadiliko yaliyoyatoa maumbo ya ndani ya vitenzi vya Kipemba (*a-e-piga, wa-e-piga*) hadi maumbo ya nje (*epiga na wepiga*) ni *udondoshaji*. Jedwali Na. 16 lifuatalo linaonyesha mifano ya sentensi za Kipemba zenye vitenzi vinavyoonyesha njeo ya wakati uliopita yakinishi kwa nafsi ya tatu umoja na uwingi.

Jedwali 4.11: Tofauti ya Sentensi za Kipemba zenye Kiambishi cha Njeo ya Wakati Uliopita (yakinishi)

Lahaja ya Kipemba	Maelezo Kiswahili sanifu
-------------------	--------------------------

epiga makelele nanna ya kichaa	alipiga makelele namna ya kichaa
mama echeka mpaka	mama alicheka sana
esoma kitabuche tangu Asubuhi mpaka nchana wa Adhuhuri	alisoma kitabu chake tangu Asubuhi mpaka Adhuhuri
enuna kwani?	alinuna kwa nini?
wepiga maji mpaka wakaanguka barabarani	walipiga maji mpaka wakaanguka barabarani.
wapinzani wecheka sana waliposikia tunshindwa kwenye uchaguzi ndogo	wapizani walicheka sana waliposikia kwamba tumeshindwa kwenye uchaguzi mdogo

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Jambo jingine linalojidhihirisha katika data iliyo kwenye maelezo yahapo awali ni ujitokezaji wa kanuni ya *uyeyushaji*, iliyotawala mabadiliko ya muundo ndani na kupelekea muundo nje wa kitenzi cha Kipemba kwenye nafsi ya kwanza uwingi, nafsi ya pili umoja na nafsi ya pili uwingi. Maumbo ya vitenzi vya Kipemba kwenye nafsi hizo yanajibadisha kutoka muundo wa ndani (*tu-e-cheka*, *u-e-cheka* na *mu-e-cheka*) na kujenga muundo wa nje (*twecheka*, *wecheka* na *mwecheka*). Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2004), *Uyeyushaji* hujitokeza katika mazingira ambapo irabu / *u* / na / *i* / inakutana na irabu nyengine isiyofanana nayo katika mpaka wa mofimu. Katika vitenzi tulivyovitaja hapo juu irabu ya nyuma juu / *u* /, inakutana na irabu ya kati mble / *e* / katika mpaka wa mofu na *uyeyushaji* unatokea, ambapo irabu / *u* /, inapoteza nguvu zake na kuwa kiyeysho cha mdomo / *w* /. Irabu / *u* / kwa hapa ni irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza na ya pili uwingi na ndio kiambishi awali chenyewe kwenye nafsi ya pili umoja. Kwa kutumia

miundo nje ya vitenzi tulivyovitaja hapo juu, tunaweza kuzibainisha sentensi za Kipemba kwenye nafsi ya kwanza uwingi, nafsi ya pili uwingi na nafsi ya pili umoja kama ifuatavyo:

Jedwali 4.12: Tofauti za Miundo ya Nje, kwenye Sentensi za Kipemba Zinazoonyesha Wakati Uliopita kwa Nafsi ya Kwanza Uwingi, Nafsi ya Pili Uwingi na Nafsi ya Pili Umoja

Lahaja ya Kipemba	Maelezo Kiswahili sanifu
<i>twecheka</i> mpaka tukakojoa	tulicheka mpaka tukakojoa
<i>wecheka</i> mno!!	ulicheka mno!!
<i>mwecheka</i> usiku nzima	mulicheka usiku mzima

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Kulingana na data katika jedwali na. 17, kanuni inayotawala mabadiliko kutoka muundo wa ndani kwenda muundo wa nje kwenye vitenzi vilivyobainishwa hapo juu ni kanuni ya uyeyushaji. Kitu kimoja cha msingi na dhahiri kinajitokeza kwenye lahaja ya Kipemba, pale ambapo kitenzi kinachoonyesha nafsi ya pili umoja (*u-e-cheka*) na nafsi ya tatu uwingi (*wa-e-cheka*) kinajikuta kina umbo moja katika muundo wake wa nje, ingawa kimetofautiana katika muundo wake wa ndani. Mlingano wake kwenye muundo wa nje umetokana na sababu ya kuwepo tofauti ya kanuni za kifonolojia au kanuni za kifonofonolojia zilizojitokeza wakati wa mchakato wa mabadiliko hayo. Kitenzi cha kwanza kilitawaliwa na kanuni ya uyeyushaji (*u-e-cheka* → *wecheka*). Kanuni hii tunaweza kuianisha kiujumla kama

/ u / [w] / - / i / au kama / u / [w] / - / é /.

kwa kesi inayohusika hapa. Kitenzi cha pili kimetawaliwa na kanuni ya udondoshaji (*wa-e-cheke* → *wecheke*), inayoweza kuwasilishwa kama / a / [ɸ] /- / ɛ /. Katika kanuni hiiinafafanuliwa kama irabu /a / katika mazingira ya kufuatiliwa na irabu / e / irabu /a / hudondoka na hubaki irabu /e /. Mukadha wa mazungumzo katika tungo ndio unaoitambulisha nafsi iliyokusudiwa, kuwa nafsi ya pili umoja au nafsi ya tatu uwingi. Kwa mfano:-

Nafsi ya pili umoja: wecheke sana ulipotuona tunshindwa ntihani.

Nafsi ya tatu uwingi: wecheke sana walipotuona tunshindwa ntihani.

Kwa upande wa hali ya ukanushi, kiambishi kitumikacho kuwakilisha njeo ya wakati uliopita katika hali hiyo kwenye kitenzi cha kawaida katika lahaja ya Kipemba ni {-e-}. Data iliyomo kwenye jedwali Na.18 inawakilisha ukweli wa hayo yaliyozungumzwa na mtafiti hapo chini.

Jedwali 4.13: Vitenzi vya Kawaida Vilivyoambikwa Njeo ya Wakati Uliopita (ukanushi) kwenye Nafsi ya Kwanza hadi ya Tatu Umoja na Uwingi

Kitenzi	Nafsi	Lahaja ya Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
		M/Ndani	M/Nje	
piga	1	si- <i>e</i> -piga	sepiga	sikupiga
		ha-tu- <i>e</i> -piga	hatwepiga	hatukupiga
	2	ha-u- <i>e</i> -piga	hwepiga	hukupiga/haukupiga
ha-mu- <i>e</i> -piga		hamwepiga	hamukupiga	
3	ha- <i>e</i> -piga	hepiga	hakupiga	
	ha-wa- <i>e</i> -piga	hawepiga	hawakupiga	
cheka	1	si- <i>e</i> -cheka	secheka	sikucheka
		ha-tu- <i>e</i> -cheka	hatwecheka	hatukucheka
	2	ha-u- <i>e</i> -cheka	hwecheka	hukucheka/haukucheka
ha-mu- <i>e</i> -cheka		hamwecheka	hamukucheka	
3	ha- <i>e</i> -cheka	hecheka	hakucheka	
	ha-wa- <i>e</i> -cheka	hawecheka	hawakucheka	
soma	1	si- <i>e</i> -soma	sesoma	sikusoma
		ha-tu- <i>e</i> -soma	hatwesoma	hatukusoma
	2	ha-u- <i>e</i> -soma	hwesoma	hukusoma/haukusoma
ha-mu- <i>e</i> -soma		hamwesoma	hamukusoma	
3	ha- <i>e</i> -soma	hesoma	hakusoma	
	ha-wa- <i>e</i> -soma	hawesoma	hawakusoma	
nuna	1	si- <i>e</i> -nuna	senuna	sikununa
		ha-tu- <i>e</i> -nuna	hatwenuna	hatukununa
	2	ha-u- <i>e</i> -nuna	hwenuna	hukununa/haukununa
ha-mu- <i>e</i> -nuna		hamwenuna	hamukununa	
3	ha- <i>e</i> -nuna	henuna	hakununa	
	ha-wa- <i>e</i> -nuna	hawenuna	hawakununa	

Chanzo: Data ya uwandani (2015)

Mambo kadhaa yanajidhihirisha katika jedwali Na.18 kwenye muundo wa ndani wa kitenzi kinachoonsha njeo ya wakati uliopita, katika hali ya ukanushi kwenye nafsi mbalimbali; yaonesha kwamba lahaja ya Kipemba inatumia mofu $\{-e-\}$, kuwakilisha mofimu ya njeo ya wakati uliopita katika hali ya ukanushi. Kutokana na muktadha huo muundo wa nje na muundo wa ndani wa vitenzi vya Kipemba vinavyowakilisha njeo ya wakati uliopita katika hali ya ukanushi vinatofautiana katika lahaja ya Kipemba. Kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji imejitokeza katika kubadilisha muundo wa ndani na kuleta muundo wa nje wa kitenzi kinachoonsha nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya tatu umoja na nafsi ya tatu uwingi (*si-e-piga* → *sepiga*, *ha-e-piga* → , *ha-wa-e-piga* → *hawepiga*), kwenye lahaja ya Kipemba. Hapa tunaweza kuwasilisha maelezo yetu kwa kanuni mbili tofauti kama

$/i/$ $[\phi]$ /- / \acute{e} / kwa nafsi ya kwanza umoja na

$/a/$ $[w]$ /- / \acute{e} /.

$/a/$ $[\phi]$ /- / \acute{e} / kwa nafsi ya tatu umoja na uwingi.

Fomula ya kanuni hii imefafanuliwa kuwa irabu / a / katika mazingira ya kuatiliwa na / e / irabu / a / hudondoka na kubakia irabu / e /. Kanuni ya uyeyushaji imetumika kubadilisha muundo wa ndani wa kitenzi cha Kipemba, kinachoonsha njeo ya wakati uliopita, katika hali ya ukanushi kwenye nafsi ya kwanza uwingi na nafsi ya pili uwingi (*ha-tu-e-piga* → *hatwepiga*, *ha-mu-e-piga* → *hamwepiga*). kanuni iliyotawala mabadiliko hayo ni

$/u/$ $[w]$ /- / i / kiujumla

/ u / [w] / - / é / kwa kesi yetu hapa. Kanuni ya uyeyushaji imetokea ambapo irabu / u / katika mazingira ya kukutana na irabu / e / huwa kiyeyusho /w / kama mfano uliopo juu unavyoonekana. Kanuni mbili zimechukua nafasi katika kubadilisha muundo wa ndani wa kitenzi cha Kipemba kinachoonesha njeo ya wakati uliopita katika nafsi ya pili umoja. Kanuni iliyotangulia ni ya udondoshaji na kanuni iliyokuja baadae ni ya uyeyushaji. Kanuni ya udondoshaji imelibadilisha umbo la ndani kutoka (*ha-u-e-piga*) na kuwa (*hu-e-piga*). Kanuni ya uyeyushaji kwa upande wake, imelibadilisha umbo la ndani kutoka (*hu-e-piga*) na kuwa umbo la nje (*hwepiga*). Kanuni mbili hizi tunaweza kuziwasilisha kwa pamoja kama

$$/ a / \quad [\phi] / - / u /$$

na / u / [w] / - / é /

Fomula ya kanuni hii inafafanuliwa kuwa irabu / u / katika mazingira ya kufuatiliwa na irabu / e / irabu hizi hubadilika na kuwa kiyeyusho / w /.

Maelezo, mifano na ufafanuzi uliobainishwa hapo juu unaonyesha kwamba, kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopita katika lahaja ya Kipemba kwenye uyaikinishi na ukanushi ni $\{-e-\}$. Kanuni zinazobadilisha muundo wa ndani na kuwa muundo wa nje katika Kipemba ni udondoshaji kwenye nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja na uwingi na uyeyushaji kwenye nafsi ya kwanza uwingi na nafsi ya pili umoja na uwingi. Mabadiliko katika Kipemba hutawaliwa na kanuni ya udondoshaji kwenye nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja na wingi. Uyeyushaji hujitokeza kwenye nafsi ya kwanza uwingi na nafsi ya pili umoja na uwingi.

4.3.1 Michakato ya kimofonolojia kwenye njeo ya wakati timilifu

Katika kipengele hiki hakuna mchakato wowote wa kimofolojia unaojitokeza katika kubadilisha muundo wa ndani kwenda muundo wa nje, kwenye lahaja ya Kipemba. Hali hii ya kutokuwepo mchakato wa kimofolojia ipo kwenye hali ya uyaikinishi na ukanushi kwa pamoja. Kwa ujumla hakuna mchakato wa kimofonolojia unaojitokeza kwenye njeo ya wakati timilifu kwenye muundo wa maneno ya lahaja ya Kipemba.

Jedwali 4.14: Michakato ya Kimofonolojia kwenye Njeo ya Wakati Timilifu

<i>Kitenzi</i>	Nafsi	Lahaja ya Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
		uyakinishi	ukanushi	
piga	1	napiga	sijapiga	nimepiga sijapiga
	2	kunpiga munpiga	hujapiga hamwepiga	umepiga hamukupiga
	3	kanpiga wanpiga	hajapiga hawajapiga	hakupiga hawakupiga
cheka	1	nacheka tuncheka	sijacheka hatujacheka	sikucheka hatukucheka
	2	kuncheka muncheka	hujacheka hamujacheka	hukucheka/haukucheka hamukucheka
	3	kancheka wancheka	hajacheka hawajacheka	hakucheka hawakucheka
soma	1	nasoma tunsoma	sijasoma hatujasoma	sikusoma hatukusoma
	2	kunsoma munsoma	hujasoma hamujasoma	hukusoma/haukusoma hamukusoma
	3	kansoma wansoma	hajasoma hawesoma	hakusoma hawakusoma
nuna	1	nanuna tunnuna	sijanuna hatujanuna	sikununa hatukununa

	2	kunnuna munnuna	<i>hujanuna</i> <i>hamujanuna</i>	hukununa/haukununa hamukununa
	3	kannuna wannuna	<i>hajanuna</i> <i>hawajanuna</i>	hakununa hawakununa

Chanzo: Data ya uwandani (2015)

4.3.2 Michakato ya Kimofonolojia kwenye Njeo ya Wakati Uliopo

Michakato na kanuni zinazoathiri miundo ya ndani na kujenga miundo ya nje ya vitenzi vilivyoambikwa njeo ya wakati uliopo yakinishi ni zile zile zilizotumika kwenye 4.2.1. Tofauti kubwa na ya msingi iliyopo kwenye kitenzi kilichoambikwa njeo ya wakati uliopita na kile kilichoambikwa kiambishi cha njeo ya wakati uliopo katika Kipemba ni kwamba kwenye njeo ya wakati uliopita kitenzi cha silabi moja hutanguliwa na kiambishi kisicho na kikomo *{ku-}*, wakati ambapo kwenye njeo ya wakati uliopo kitenzi cha aina hiyo hujitokeza pekee bila kutanguliwa na kiambishi kisichokuwa na kikomo *{ku-}*, kama ilivyo kwenye jedwali na. 19 hapo juu.

Jedwali 4.15: Vitenzi vya Silabi Moja Vilivyoambikwa Njeo ya Wakati Uliopo

Kitenzi	Kipemba		Maelezo Kiswahili sanifu
	M/Ndani	M/Nje	
fa	ni-a-fa	nafa	nnakufa
	tu-a-fa	twafa	tunakufa
	u-a-fa	wafa	unakufa
	mu-a-fa	mwafa	munakufa
	a-a-fa	afa	anakufa
	wa-a-fa	wafa	wanakufa

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Data ya hapo juu inaonyesha kuwa kwenye hali ya ukanushi katika vitenzi vya Kipemba, hakuna ufungamani wa kanuni yoyote ya kimofonolojia, isipokuwa kanuni ya $z+(-i)$ inayowakilisha hali ya ukanushi kwenye kitenzi kinachoashiria njeo ya wakati uliopo, hulazimisha irabu ya mwisho iwe / i / badala ya irabu $\{a\}$ kama ilivyo kwenye hali ya uyakinishi. Kwa ujumla kwenye njeo ya wakati uliopo michakato ya kimofonolojia hujitokeza kwenye uyakinishi tu wa kitenzi cha lahaja ya Kipemba, kwenye ukanushi wa kitenzi cha Kipemba hakuna mchakato wa aina hii.

4.3.3 Michakato ya Kimofonolojia kwenye Hali ya Kudadisi kwa Tendo

Kama tulivyoona kwenye maelezo ya hapo juu, kiambishi kinachowakilisha hali ya kudadisi kwa tendo kwenye Kipemba ni $\{-enge /-engeli /-engali\}$ kwenye uyakinishi na $\{-senge /-sengeli /-sengali\}$ kwenye ukanushi. Maumbo haya huathiri mabadiliko kutoka muundo wa ndani kwenda muundo nje. Mabadiliko ya muundo wa ndani yanayoleta muundo mpya wa nje yanajitokeza kwenye Kipemba katika hali ya uyakinishi. Hayajitokezi kwenye ukanushi. Mabadiliko yajitokezayo kwenye lahaja ya Kipemba kwenye hali ya uyakinishi hujitokeza kupitia kanuni za udondoshaji na uyeyushaji kama itakavyobainika hapo chini. Kanuni hizi zimebainishwa na mtafiti kama ilivyo hapo chini:-

Jedwali 4.16: Michakato ya Kimofonolojia kwenye Hali ya Kudadisi kwa tendo

Kitenzi	Nafsi	Lahaja ya Kipemba			Maelezo Kiswahili sanifu	
		Uyakinishi		Ukanushi	Uyakinishi	Ukanishi
		M/Ndani	M/Nje			
piga	N 1 - umoja	Ni- <i>e-ngepig</i> a	<i>nengepiga</i>	<i>nisengepiga</i>	<i>ningepiga</i>	<i>nisingepiga</i>
	N1-uw ingi	Tu- <i>e-ngepi</i> ga	<i>twengepiga</i>	<i>tusengepiga</i>	<i>tungepiga</i>	<i>tusingepiga</i>
	N 2 - umoja	<i>uengepiga</i>	<i>wengepiga</i>	<i>usengepiga</i>	<i>ungepiga</i>	<i>usingepiga</i>
	N2-uw ingi	<i>muengepiga</i>	<i>mwengepiga</i>	<i>musengepiga</i>	<i>mungepiga</i>	<i>musingepiga</i>
	N 3 - umoja	<i>aengepiga</i>	<i>engepiga</i>	<i>asengepiga</i>	<i>angepiga</i>	<i>asingepiga</i>
	N3-uw ingi	<i>waengepiga</i>	<i>wengepiga</i>	<i>wasengepiga</i>	<i>wangepiga</i>	<i>wasingepiga</i>

Chanzo: Data ya Uwandani (2015)

Kwa ujumla kwenye njeo ya wakati uliopo michakato ya kimofonolojia hujitokeza kwenye uyakinishi wa kitenzi cha lahaja ya Kipemba tu, kwenye ukanushi wa kitenzi cha Kipemba hakuna mchakato wa aina hii.

4.3.4 Michakato ya Kimofonolojia kwenye Vitenzi vya Hali ya Mazoea.

Mabadiliko ya muundo wa ndani kwenda muundo wa nje yamejitokeza kwenye Kipemba kwenye hali ya uyakinishi tu. Hakuna mabadiliko kwenye ukanushi wa lahaja ya Kipemba . Namna mchakato huu unavyojitokeza na unavyofanya kazi imefafanuliwa kwa kina katika maelezo ya hapo awali kwa kuwa kitenzi cha wakati

uliopo uyakinishi kwenye Kipemba unalingana na ule wa hali ya mazowea katika lahaja hiyo.

4.4 Kanuni Zitumikazo Kugeuza Miundo Ndani kwenda Miundo Nje

Miundo ya ndani ya vitenzi vya Kiswahili huathiriwa na kanuni na michakato tofauti tofauti kwa kupitia kanuni na kaida mbalimbali. Lengo la msingi la kipengele hiki ni kubainisha kanuni mbalimbali zinazoongoza mabadiliko kutoka miundo ya ndani kwenda miundo ya nje.

4.4.1 Kanuni Zitumikazo kwenye Njeo ya Wakati Uliopita

Kanuni zitumikazo kwenye njeo ya wakati ulipita kwenye nafsi mbalimbali ni udondoshaji na uyeyushaji.

4.4.1.1 Udondoshaji

Udondoshaji kwenye lahaja ya Kipemba katika uyakinishi umejitokeza kwenye nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya tatu umoja na uwingi. Kwenye nafsi ya kwanza kinachodondoka ni /i/, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja; $\{ni-e-piga \rightarrow nepiga\}$ ambayo inaweza kuwasilishwa kama

/ i / [ϕ] / - / \acute{e} /. Kwenye nafsi ya tatu umoja kinachodondoka in { a-}, kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya tatu umoja $\{a-e-piga \rightarrow epiga\}$, ambayo inaweza kuwasilishwa kama / a / [ϕ] / - / \acute{e} /. Kwenye nafsi ya tatu uwingi kinachodondoka in / a /, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya tatu uwingi $\{wa-e-piga \rightarrow wepiga\}$ ambayo inaweza kuwasilishwa kanuni ifuatayo

/ a / [ϕ] / - / é / .

Kwenye ukanushi katika lahaja ya Kipemba, udondoshaji hujitokeza kwenye nafsi ya kwanza umoja nafsi ya pili umoja. Kwenye nafsi ya kwanza umoja, kinachodondoka ni /i/, irabu ya kiambishi awali cha ukanushi kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja; {*si-e-piga* → *sepiga*} ambayo inaweza kuwasilishwa kwa kanuni ya

/ i / [ϕ] / - / é / . Kwenye nafsi ya tatu umoja. Kwenye nafsi ya tatu umoja, kinachodondoka ni irabu mbili za /a /, irabu ya kiambishi cha ukanushi na irabu nyingine /a /, ambayo ni kiambishi nafsi ya tatu umoja {*ha-a-epiga*-- → *hepiga*}, ambayo inaweza kuwasilishwa kwa kanuni ifuatayo kufafanuliwa kama irabu / a / katika mazingira ya kukutana na irabu / a / hivyo basi irabu / a / hudondoka na kubaki irabu / a / moja tu kama fomula iliyopo chini inavyooneka.

/ a / [ϕ] / - / é / .

4.4.1.2 Uyeyushaji

Uyeyushaji hujitokeza kwenye nafsi ya kwanza uwingi, nafsi ya pili umoja na nafsi ya pili uwingi. Kwenye nafsi ya kwanza uwingi uyeyushaji hujitokeza pale ambapo irabu ya juu nyuma /u/, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza uwingi; {*tu-e-piga* → *twepiga*}. Kwenye nafsi ya pili umoja uyeyushaji hujitokeza pale ambapo irabu ya juu nyuma /u /, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya pili umoja; {*mu-e-piga* → *mwepiga*}. Kwenye nafsi ya tatu uwingi uyeyushaji

hujitokeza pale ambapo irabu ya juu nyuma /u /, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya pili uwingi. Kanuni ya jumla inayowakilisha uyeyushaji ni / u / [w] / - / é /.

Kuna mambo mawili makubwa ya kuzingatia. Jambo la kwanza ni kwamba, kwenye nafsi ya pili umoja kumejitokeza kanuni mbili zinazofanya kazi kwa pamoja. Kanuni ya udondoshaji, inayofuatiwa na kanuni ya uyeyushaji. Udondoshaji huligeuza umbo la ndani kutoka {ha- u-e-piga} mpaka {hu-e-piga} na uyeyushaji hulitoa umbo la ndani kutoka {hu-e-piga} na kutengeneza umbo la nje {hwepiga} . Ambayo inaweza kuwasilishwa kama / u / [w] / - / é /

Jambo la pili la kuzingatia ni kwamba kwenye nafsi ya kwanza uwingi, nafsi ya pili umoja na nafsi ya tatu uwingi hakujitokezi athari yoyote mpya iliyotokana na kiambishi cha ukanushi {ha-}. Baada ya kuambikwa kiambishi hiki maumbo ya vitenzi hubaki kama yalivyo sawa na yalivyoathiriwa na kanuni zilezile zilizotajawa kwenye uyakinishi.

Kwa ujumla kanuni zinazotawala mabadiliko kutoka muundo wa ndani kwenda muundo wa nje ni *udondoshaji* na *uyeyushaji*.

4.4.2 Kanuni Zinazotumika kwenye Njeo ya Wakati Timilifu na Wakati Ujao

Kwa mujibu wa data iliyopatikana kitenzi cha Kipemba kilichoambikwa njeo inayowakilisha wakati timilifu na wakati ujao hakina mabadiliko kati ya muundo wa

ndani na muundo wa nje kwenye uyaikinishi na kwenye ukanushi. Kwa mantiki hii inaonekana kwamba hakuna kanuni yoyote inayotawala mabadiliko kati ya muundo ndani na muundo nje.

Jedwali 4.17: Kiambishi Kinachowakilisha Njeo ya Wakati Timilifu na Wakati

Ujao

Kitenzi	Nafsi	Lahaja ya Kipemba	Maelezo Kiswahili sanifu
lia	N1-umoja	nnalia	nimelia
	N1-uwingi	tunalia	tumelia
	N2-umoja	unalia	umelia
	N2-uwingi	munalia	mumelia
	N3-umoja	anacheza	amecheza
	N3- umoja	wanacheza	wamecheza

Chanzo: Data ya uwandani (2015)

4.4.3 Kanuni Zinazotumika kwenye Njeo ya Wakati Uliopo

Kama ilivyo kwa wakati uliopita, kanuni zinatumika kwenye njeo za wakati uliopo katika Kipemba ni udondoshaji na uyeyushaji. Kwa ujumla kanuni hizi zinaweza kubainika kwenye vitenzi vilivyoambikwa njeo hiyo ya wakati uliopo katika uyaikinishi na ukanushi kwa kuzingatia mtiririko maalumu.

Kitenzi kilichoambikwa nafsi ya kwanza umoja katika Kipemba uyaikinishi $\{ni-a-piga \rightarrow napiga\}$, katika mchakato huu kanuni ya udondoshaji imetumika hapa

na kilichodondoka ni /i/, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja. Kanuni ya mchakato huu ni / i / [Φ] / - / a /

Iwapo kitenzi kitaambikwa nafsi ya kwanza uwingi katika hali ya uyaakinishi kwenye Kipemba {*tu-a-piga* \rightarrow *twapiga*}, kanuni ya uyeyushaji hutumika hapa na kanuni hii husababishwa na mvutano wa irabu /u/ na irabu /a / kwenye mpaka wa mofu mbili. Jambo hili huilazimisha irabu /u/, kuyeyuka na kuwa /w/; kiyeyusha cha midomo. Kanuni hii husababishwa na mkutano wa irabu / u / na irabu / a/ kwenye mpaka wa mofu mbili {*u-a-piga* \rightarrow *wapiga*}. Mvutano huu husababisha irabu /u / kuyeyuka na kuwa /w/; kiyeyusha cha midomo kama fomula hii inavyobainisha . Kanuni ya uyeyushaji inajitokeza pia kwenye kitenzi kilichoambikwa kiambishi awali cha nafsi ya pili uwingi, ambapo irabu /u/ huyeyuka na kuwa /w/; kiyeyusha cha midomo kwenye mkutano wa irabu /u/ na irabu /a/ kwenye mpaka wa mofu mbili. Umbo la kitenzi linageuka kutoka {*mu-e-piga* \rightarrow *mwepiga*}. Iwapo kitenzi kitaambikwa kiambishi nafsi ya tatu umoja na uwingi kanuni ya *udondoshaji* hujitokeza. Kinachodondoka katika mazingira haya ni irabu /a/. *Udondoshaji* huu hujitokeza pale ambapo irabu mbili zinazofanana hukutana kwenye mpaka wa mofu mbili; {*a-a-piga* \rightarrow *apiga*, *wa-a-piga*- \rightarrow *wapiga*}. Kwa hiyo kanuni ya

/ a / [Φ] / - / i / inabainisha hilo Kutokana na hali hiyo irabu / a / katika mazingira ya kukutana na irabu / a / irabu /a / moja hudondoka na kubaki irabu / a / moja kama fomula inavyooneka juu. Kwa maelezo zaidi hakuna kanuni yoyote iliyotawala mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje. Kwa hivyo

maumbo ya vitenzi vilivyoambikwa njeo ya wakati uliopo hayabadiliki kwenye muundo ndani na muundo nje.

4.4.4 Kanuni za Mabadiliko ya Kimofonolojia katika Muundo wa Vitenzi vya Lahaja ya Kipemba (kudadisi kwa tendo)

Kwa mujibu wa data zilizopatikana katika hali ya kudadisi kwa tendo kwenye lahaja ya Kipemba kama zinavyoonekana katika jedwali na. 11, kanuni zinazobadilisha miundo ya ndani kwenda miundo ya nje zinajitokeza kwenye hali ya uyaikinishi tu. Kwenye ukanushi wa hali ya kudadisi kwa tendo wa Kipemba ukanushi hakuna kauli yeyoyote inayojitokeza.

Kitenzi kilichoambikwa nafsi ya kwanza umoja katika Kipemba uyaikinishi {*ni-enge-piga* → *nengepiga*}, kanuni ya udondoshaji imetumika hapa na kilichodondoka ni /i/, irabu ya kiambishi awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja. Iwapo kitenzi kitaambikwa nafsi ya kwanza uwingi katika hali ya uyaikinishi kwenye Kipemba mfano: Neno {*tu-enge-piga* → *twengepiga*} kama inavyobainishwa na kanuni ya uyeyushaji itumikayo hapa ni

/u/ [w] /- /é /.

Kanuni hii husababishwa na mkutano wa irabu /u/ na irabu /e/ kwenye mpaka wa mofu mbili. Jambo hili huilazimisha irabu /u/, kuyeyuka na kuwa /w/; kiyeyusha cha midomo. Iwapo kitenzi cha kawaida cha Kiswahili kitaambikwa kiambishi nafsi ya pili umoja katika Kipemba kwenye hali ya uyaikinishi kanuni ya uyeyushaji hutumika.

Kanuni hii husababishwa na mkutano wa irabu /u/ na irabu /e/ kwenye mpaka wa mofu mbili $\{u\text{-enge-piga} \rightarrow wengepiga\}$. Mkutano huu husababisha irabu /u/ kuyeyuka na kuwa /w/; kiyeyusho cha midomo. Kanuni ya uyeyushaji inajitokeza pia kwenye kitenzi kilichoambikwa kiambishi awali cha nafsi ya pili uwingi, ambapo irabu /u/ huyeyuka na kuwa /w/; kiyeyusho cha midomo kwenye mkutano wa irabu /u/ na irabu /e/ kwenye mpaka wa mofu mbili. Umbo la kitenzi linageuka kutoka $\{mu\text{-enge-piga} \rightarrow mwengepiga\}$. Iwapo kitenzi kitaambikwa kiambishi nafsi ya tatu umoja na uwingi kanuni ya *udondoshaji* hujitokeza. Kinachodondoka katika mazingira haya ni irabu / a /. *Udondoshaji* huu hujitokeza pale ambapo irabu /a/ hukutana na irabu /e/ kwenye mpaka wa mofu mbili; $\{a\text{-enge-piga} \rightarrow engepiga, wa\text{-enge-piga} \rightarrow waengepiga\}$. Kanuni hii imebainishwa kama ifuatavyo / a /

[Φ] / - / é /. Fomula ya kanuni hii inaeleza irabu /a / katika mazingira ya kufuatana na irabu / e / irabu / a / hudondoka na kubakia irabu / e / kama mfano wa fomula inavyooneka juu.

4.4.5 Kanuni Zitumikazo kwenye Hali ya Mazoea

Kitenzi cha hali ya mazoea uyakinishi katika Kipemba ni sawa sawa na kitenzi kilichoambikwa njeo ya wakati uliopo ambayo imeelezwa katika kipengele cha 4.2.

3. Michakato ya kimabadiliko na kanuni zake hazitofautiani na zile zilizoainishwa na kwa upande mmoja na. 4.3.3 kwa upande wa pili. Kwenye hali ya ukanushi kwenye lahaja hii hakuna mabadiliko na kwa hivyo hakuna mchakato wa kimofolojia wala kanuni zinazotwala mabadiliko hayo.

4.4.6 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii mtafiti anawasiisha na kujadili data za utafiti zilizokusanywa kwa kuangalia viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba katika kubainisha muundo ndani na muundo nje, kubainisha michakato ya kimofonolojia katika muundo ndani na muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba na kubainisha kanuni za kimofonolojia zinazotawala mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Katika sura hii kuna ubainishaji wa viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba katika wakati uliopo, wakati uliopita, wakati ujao, hali timilifu, wakati wa mazoea na wakati wa kudadisi tendo katika kuzingatia hali ya uyaakinishi na ukanushi.

SURA YA TANO

MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Muhutasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza “Viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba ” ambapo ulikuwa na malengo matatu ambayo ni kuchunguza viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba. Kueleza michakato ya kimofonolojia inayojitokeza katika kubadilisha miundo ya ndani kwenda miundo ya nje ya vitenzi kwenye lahaja ya Kipemba na kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko kutoka muundo wa ndani kwenda muundo wa nje kati ya lahaja ya Kipemba. Utafiti huu ulifanyika katika Kisiwa cha Pemba, kwenye Shehia ya Mtambwe Kaskazini, katika kijiji cha Kele, Uondwe, Mpakanjia, Nyali , Kiapaka na Chanjaani .

Jumla ya wazungumzaji asilia wa Kipemba ni sitini (60) ndio walishiriki katika utafiti huu ambao ni wenye umri wa zaidi ya miaka sitini (60). Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji/dodoso, usaili na uchunguzi makini. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa njia ya maelezo na majedwali yalitumika kwa nadra sana pale yalipohitajika.

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya fonolojia zalishi iliyoasisiwa na Noam Chomsky (1957) na kutumiwa na wanaisimu wengi waliofanya kazi za isimu na ambao wameelezea viambishi njeo kama Maganga (1995) na Salma.

5.2 Muhutajari wa Matokeo ya Utafiti

a) Kuhusu lengo la kwanza la utafiti lililolenga kubainisha viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba, utafiti huu umebaini kuwa, kuna tofauti kidogo baina ya viambishi vinavyowakilisha njeo mbalimbali za nyakati baina ya lahaja za Kipemba i) Njeo ya wakati uliopita kwenye Kipemba hua kiambishi $\{-e-\}$ kwenye uyaikinishi na ukanushi, ilhali kwenye ii) Njeo ya hali timilifu kwenye lahaja ya Kipemba hua kiambishi $\{-n(a)\}$ kwenye uyaikinishi na kiambishi $\{-ja-\}$ kwenye ukanushi, ilhali , iii) Njeo ya wakati uliopita kwenye lahaja ya Kipemba hua kiambishi $\{-a-\}$ kwenye uyaikinishi na kipashio $z+(-i)$ kwenye ukanushi.

b) Kuhusu lengo la pili ambalo lililenga kueleza michakato ya kimofonolojia inayojitokeza katika njeo za vitenzi ambapo imedhihirika kuwa lahaja ya Kipemba huruhusu michakato ya kimofonolojia inayopelekea mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje kwenye vitenzi mbalimbali. Michakato ya kimabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje kwenye lahaja ya Kipemba hujitokeza dhahiri kwenye nyakati zinazofuata hapo chini.

- (i) Vitenzi vya lahaja ya Kipemba vilivyoambikwa njeo ya wakati uliopita uyaikinishi na ukanushi

- (ii) Vitenzi vya lahaja ya Kipemba vilivyoambikwa njeo ya wakati uliopo uyakinishi.
 - (iii) Vitenzi vya lahaja ya Kipemba vilivyoambikwa viambishi vya hali ya kudadisi kwa tendo uyakinishi na
 - (iv) Vitenzi vya lahaja ya Kipemba vilivyoambikwa viambishi vya hali ya mazoea uyakinishi.
- c) Lengo la tatu la utafiti huu, lilihusu kubainisha kanuni zinazotawala mabadiliko kutoka muundo ndani kwenda muundo nje katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba ambapo michakato iliyotawala mabadiliko hayo ya miundo ndani kwenda miundo nje hujitokeza kupitia kanuni mbili kuu, ambazo ni udondoshaji na uyeyushaji. Udondoshaji katika viambishi njeo hutawala mabadiliko kwenye vitenzi vilivyoambikwa nafsi za kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja na uwingi, ilhali uyeyushaji umejikita zaidi kwenye nafsi ya kwanza wingi, na nafsi ya pili umoja na uwingi.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu umedhihirisha mabadiliko na michakato mbalimbali ambayo hujitokeza katika muundo wa vitenzi vya lahaja za Kipemba katika kudhihirisha nyakati mbalimbali pamoja na michakato inayobadilisha miundo ndani na miundo nje, lakini waongaji wa lahaja za Kipemba wanafahamiana vizuri sana katika mawasiliano yao japokuwa wanatofautiana kiusemaji.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Ni mtazamio ya mtafiti wa uchunguzi huu kuwa kazi hii itatoa mchango wa pekee kuhifadhi kipengele cha fonolojia cha lahaja ya Kipemba, kwa sababu hiyo mtafiti wa kazi hii anapendekeza kuwa, wataalamu wa lugha ya Kiswahili waendeleze juhudi hii kwa kuandika tafiti nyingine zinazohusu vipengele vingine vya kiisimu vinavyohusu njeo katika vitenzi vya lahaja mbali mbali za Kiswahili. Tafiti hizi kwa ujumla wake zitaimarisha jitihada za kuhifadhi lahaja za Kiswahili. Kwa upande mwingine, zitawasaidia walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili katika ngazi mbali mbali za elimu kama shule za sekondari, vyuo na hata vyuo vikuu kupata marejeleo ya kujifunzia na kufundishia. Hapa chini ninatoa mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji na kwa utafiti zaidi wa lahaja za Kipemba.

5.4.1 Mapendekezo ya Utekelezaji

Ili kuhakikisha kuwa lahaja za Kipemba zinadumishwa, Wizara ya elimu ihimise matumizi ya lahaja hizi katika jamii na iweke katika muhtasari wake mafunzo yanayohusu lahaja mbali mbali za Kipemba.

5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Nyingine

Mtafiti anapendekeza tafiti zaidi zifanywe katika vipengele vingine vya fonolojia na muundo wa lahaja ya Kipemba na lahaja nyingine za Kiswahili; kama vile kuchunguza viambishi nafsi na viambishi nyambulishi vilivyoko katika lahaja ya Kipemba. Tafiti hizi kwa ujumla wake zitawasaidia wataalamu wa lugha katika

Wizara ya elimu, baraza la mitihani na taasisi za utafiti wa Kiswahili kuangalia namna lahaja hizi zinavyoweza kuwa chimbuko la maendeleo ya Kiswahili kwa jumla na njia ya kuboresha mitaala ya mafunzo ya Kiswahili. Vilevile itawasaidia walimu wa ngazi mbalimbali kama vyuo hata vyuo vikuu kupata marejeleo ya kujifunzia na kufundishia.

MAREJELEO

- Adam, J. and Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Graduate Business and Social Studies*. Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Chomsky, N. (1957). *Some General Properties of Phonological Rules*. *Language*, 43(1), 102-128. doi:1. Retrieved from <http://www.jstor.org/stable/411387> doi:1, date 22.August. 2016.
- Enon, J.C. (1998). *Research methods in special education and field study*. London. Oxford
- Goldsmith, John. A. (1995). *Phonological Theory*. In John A. Goldsmith (1995). *The Handbook of Phonological Theory*. *Blackwell Handbooks in Linguistics*. Malden MA. Blackwell Publishers.

- Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.
- Hamad, S. O. (2011). *Tense Aspect Dissertation*. (Unpublished Thesis). Dar es Salaam. University of Dar es Salaam.
- Hayes, B. (2009). *Introductory phonology*. Malden, MA: Wiley-Blackwell.
- Kamusi ya Kiswahili sanifu, (2004). *Kamusi ya Kiswahili. Toleo la 2*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- Kihore, Y. M. na wenzake. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA)*. TUKI. Dar es Salaam.
- Kombo, D. K. na Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An introduction*. Paulines Publishers. Nairobi.
- Kothari, C. K. (2004). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi Wiley.
- Maganga, C. (1995). *A study of morphophonology of standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi*. (Unpublished PhD. Thesis) University of Dar- es- Salaam.
- Massamba, D. P. B. na wenzake (2003). *Historia ya Kiswahili 50 BK hadi 1500BK*. The Jomo Kenyatta University. Nairobi.
- Mathooko, P. M. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi. Njiku Books, Kenyatta University.
- Mazrui, M.A. (1983). *Aspect marking in Swahili: According to Variation*. TUKI. Dar es Salaam.

- Mekacha, D. K. (2000), *Isimu Jamii: Nadharia na muktadha wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi, Longhorn Publishers: Nairobi.
- Mkude, D. J. (1983). *Mtawanyiko wa makala za za semina ya Kimataifa ya waandishi WA Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI.
- Polome, E.C. (1967). *Swahili language Handbook. Center for Applied linguistics*. Washington.
- Salma, R. (2011). *Tense and Aspect representation in Pemba Dialect*. (Unpublished thesis), University of Dar es Salaam.
- Saucloux, C. (1909). *Grammar of Dialectal Changes in the Kiswahili language*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Schutt, K. R. (2006). *Investigating the Social World. The process of Education Research 5th*. Thousand Oaks: Pine Forge Press.
- Steere, E. (1930). *A handbook of the Swahili Languages as spoken as Zanzibar*. Cambridge University Press. London.
- Suwed, A. A. (2012). *Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa matumizi ya lugha katika filamu za Steven Kanumba*. (Tasnifu ya umahiri haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salaam.
- TUKI, (1990). *Kamusi ya Isimu ya lugha*. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Walliman, N. (2011). *Research methods: The basics*. London: Routledge

Whitley, W. H. (1958). *The Dialects and verse of Pemba: An introduction*. Kampala: East African Swahili Committee, Makerere College (*Kimtang'ata in Swahili Dialects-1*). Nairobi. EAPH.

KIAMBATANISHO 1

Orodha ya dodoso la utafiti

Jina la mtafiti..... (iwapo atapenda kulibainisha jina lake) .

Umri

Jinsia..... mke / mume.

Njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba	Maelezo Kiswahili sanifu
Napiga	ninapiga
Twapiga	tunapiga
Wapiga	wanapiga
Mwapiga	munapiga
Apiga	anapiga
Wapiga	wanapiga
Necheza	nilicheza
Twecheza	tulicheza
Wecheza	ulicheza
Mwecheza	mulicheza
Echeza	alicheza
Wecheza	walicheza
Ntasoma	nitasoma
Tutasoma	tutasoma

Utasoma	utasoma
Mtasoma	mutasoma
Atasoma	atasoma
Watasoma	watasoma
Nnaimba	nimeimba
Tunaimba	tumeimba
Unaimba	umeimba
Mnaimba	mumeimba
Anaimba	ameimba
Wanaimba	wameimba
Nacheza	ninacheza
Twacheza	tunacheza
Wacheza	wanacheza
Mwacheza	munacheza
Acheza	anacheza
Wacheza	wanacheza
Nengefika	nengefika
Twengefika	tungefika
Wengefika	wengefika
Mwengefika	mungefika
Engefika	engefika
Wengefika	wengefika

KIAMBATANISHO 11**Majibu ya Watafitiwa****Jina la mtafitiwa..... (iwapo atapenda kulibainisha jina lake)****Umri****Jinsia.....Mke / Mume.****Kiambishi njeo katika lahaja ya Kipemba Maelezo Kiswahili sanifu**

Napiga	ninapiga
Twapiga	tunapiga
Wapiga	wanapiga
Mwapiga	munapiga
Apiga	anapiga
Wapiga	wanapiga
Necheza	nilicheza
Twecheza	tulicheza
Wecheza	ulicheza
Mwecheza	mulicheza
Echeza	alicheza
Wecheza	walicheza
Ntasoma	ntasoma
Tutasoma	tutasoma
Utasoma	utasoma

Mtasoma	mutasoma
Atasoma	atasoma
Watasoma	watasoma
Nnaimba	nimeimba
Tunaimba	tumeimba
Unaimba	umeimba
Mnaimba	mumeimba
Anaimba	ameimba
Wanaimba	wameimba
Nacheza	ninacheza
Twacheza	tunacheza
Wacheza	wanacheza
Mwacheza	munacheza
Acheza	anacheza
Wacheza	wanacheza
Nengefika	nengefika
Twengefika	tungefika
Wengefika	wengefika
Mwengefika	mungefika
Engefika	engefika
Wengefika	wengefika